# Nipashe

Ijumaa Septemba 16, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581070

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAM

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 7007

LIKE & FOLL



SUPA JACKPOT

TZS. 1,031,243,893

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




**Kampuni** za kigeni 75 zatafuta fursa uwekezaji nchini

UKURASA 4



**JOSHUA NA TYSON KUZICHAPA DESEMBA**

UKURASA 22



# Wabunge wacharuka kukithiri Panya Road

• **Wataka** muda walijadili kwa kina, Spika aipa serikali... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 19

**ABIRIA MWINGINE WA KENYA AIRWAYS AFARIKI DUNIA**

SHIRIKA la Ndege la Kenya Airways limethibitisha kuwa abiria mmoja alipata matatizo ya kupumua alipokuwa akipanda moja ya...

## Biashara ya chenji yazidi kushika kasi

UKURASA 3




Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba (wa pili kushoto) na Ofisa Mkuu wa Wateja Wakubwa wa Benki ya NMB, Alfred Shayo, wakizindua tawi jipya la NMB Ngamiani, jijini Tanga jana. Kulia ni Meneja wa benki hiyo, Kanda ya Kaskazini, Dismas Prosper na Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Henry Shekifu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rais Samia avunja ukimya mikutano vyama vya siasa

UKURASA 3

**MICHEZO** **MASTRAIKA YANGA WATAFUTIWA DAWA** UK.24 **KABWELA** UK.18

# Katekista mbaroni madai ya kumnajisi mtoto miaka minane

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

JESHI la Polisi mkoani Geita linamshikilia Katekista Athanas Agustino (62), wilayani Chato kwa tuhuma ya kumnajisi mwanafunzi wa darasa la tatu mwenye umri wa miaka minane.

Kamanda wa Polisi mkoani Geita, Henry Mwaibambe akizungumza na waandishi wa habari jana alisema tukio hilo lilitokea Agosti 4, mwaka huu.

Alisema mtuhumiwa huyo alimvizia mtoto huyo ofisini kwake, alipokwenda kusoma mafundisho ya dini na kisha kumfanyia ukatili huo.

Mwaibambe alisema katika mahojiano na mtuhumiwa huyo baada ya kutiwa nguvuni, alikiri kumfanyia ukatili mtoto huyo.

Alisema mtuhumiwa huyo atafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika ili kujibu mashtaka yanayomkabili.

"Baada ya mtuhumiwa huyo kukamatwa alikiri kumfanyia ukatili mtoto huyo na kuomba msamaha, atafikishwa mahakamani ushahidi utakapokamilika," alisema.

Wakati huo huo, Jeshi hilo linamshikilia James Mtogori (28), mkazi wa Katoro mkoani humo, mlinzi wa kampuni ya KACHIPA kwa tuhuma ya kumjeruhi kwa risasi sehemu za mwili Kulwa Silvesta (26), mkazi wa Katoro.

Mwaibambe aliwataka wananchi wa mkoa huo wanaomiliki silaha kinyemela kuzisalimisha haraka ifikapo Oktoba 30, mwaka huu.

# ... Dar hali bado si shwari

**Na Waandishi Wetu**

HALI ya usalama Dar es Salaam si shwari kutokana na kundi la watoto wenye umri kati ya miaka 14 na 17 maarufu kama 'Panya Road' kuendelea kufanya uhalifu katika maeneo mbalimbali.

Vijana hao wamevamia mtaa wa Majimatitu A, Kata ya Mianzini, wilaya ya Temeke usiku na kumjeruhi kijana wa ulinzi shirikishi, Mohamed Mpondela (52) kwa kumkata panga kichwani kisha kupora mali mbalimbali.

Ofisa Uhusiano wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), Patrick Mvungi, jana alithibitisha kupokewa kwa majeruhi huyo katika taasisi hiyo na kwamba anaendelea na matibabu na amefanyiwa upasuaji.

Mkuu wa Vikundi vya Ulinzi Shirikishi Majimatitu, Salum Abdallah, alisema tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia Jumanne, baada ya vijana hao waliokuwa zaidi ya 20, kuvamia maeneo hayo wakiwa na silaha za jadi.

Alisema baada ya kufika eneo hilo, baadhi waliingia kwenye nyumba moja na wengine walibaki nje ndipo vijana wa ulinzi shirikishi walipowabaini na wakati wakikabiliana nao, mlinzi mmoja alijeruhiwa kwa kupigwa panga eneo la fuvu la kichwa.

"Walikuwa zaidi ya vijana 20 maana yake hawa ni 'Panya Road'. Walipofika maeneo haya walivamia nyumba ya kwanza wakaja nyumba ya pili, tukio lilitokea majira kama ya saa 9:30 usiku. Wakakutana na makamanda wangu walikuwa kama 15 hawakuwa mbali walipowaona waliwafuata, ndipo wakaanza purukushani.

"Kwa bahati mbaya makamanda wangu wakawa wamezidiwa nguvu, wale wakawa wako wengi ndipo kamanda wangu mmoja akajeruhiwa na ile nyumba waliyovamia mtoto wa mwenye nyumba amekatwa panga la mkononi. Walifanikiwa kuondoka na televisheni mbili na walikwenda upande wa Mzambarauni," alisema.

Usiku wa kuamkia juzi, alisema waliimarisha doria maeneo hayo, wakapata taarifa kikundi hicho kimevamia Chamanzi maeneo ya Mkondogwa, Dovya.

"Inavyoonekana hawa vijana wapo wengi, bahati nzuri tulikuwa na redio tukawa tunawasiliana baada ya kufurumushwa huko wakakimbilia maeneo ya kwetu na kwa sababu tulikuwa tayari tumeshatoa taarifa kituo cha polisi, tukawa tumejipanga maeneo ya bonde la Muhimbili.

"Tulifanikiwa kuwazingira vijana kama watatu lakini namna walivyotutoka hatukuelewa, hatukufanikiwa kuwahoji, ilikuwa kama saa tisa usiku, umri wao ni kuanzia miaka 14 hadi 17. Chamanzi hawakufanikiwa kuiba chochote kwa sababu tuliimarisha ulinzi, tulipiga wameelekea wapi," alisimulia.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, akizungumza na wananchi wa Chanika kata ya Zingiziwa, wilaya ya Ilala, jana alisema mzazi mwenye mtoto 'Panya Road' kuanzia siku hiyo, asipomuona nyumbani asihangaike akamtafute Kituo cha Polisi au hospitali.

Makalla alitangaza kukamatwa kwa watuhumiwa wengi katika tukio laTabata, Kawe, na Mizimuni na kueleza wengi ni waliotoka gerezani na kumaliza vifungo, na kuiomba mahakama kwa wale makosa yao yanajirudia hukumu yao iwe kali zaidi.

Nipashe ilipomtafuta Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, kuzungumzia kuhusu tukio hilo, aliomba apewe muda ili afuatilie.

**Imeandaliwa na Romana Mallya, Pillly Kigome (Dar)**




Mbunge wa Ubungo, Prof. Kitila Mkumbo (kulia), akichangia mjadala kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Demokrasia Duniani na miaka 30 ya urejeshwaji wa mfumo wa vyama vingi nchini, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mwenyekiti wa Chama cha wananchi (CUF) Taifa, Prof. Ibrahimu Lipumba (wa pili kulia), Mbunge wa Viti Maalum CCM, Neema Rugangira (wa tatu kulia) na Mchokoza mada, Wakili wa Kujitegemea, Lulu Urio. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wabunge wacharuka kukithiri Panya Road

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

VITENDO vya uhalifu vinavyofanywa na makundi maarufu ya Panya Road na Watu Kazi, vimewaibua wabunge na kuitaka serikali kuchukua hatua madhubuti kuyadhibiti kwa kuwa yanatishia maisha na usalama wa raia na mali zao.

Kutokana na kukithiri kwa vitendo hivyo katika maeneo mbalimbali nchini, ikiwamo Dar es Salaam, jana Wabunge Bahati Ngindo (Viti Maalum- CCM) na Bonna Kamoli (Segerea- CCM) walisimama na kuomba mwongozo kwa Spika.

Katika mwongozo huo, wabunge hao waliomba Bunge liahirishe ratiba yake na badala yake lijadili jambo la dharura kuhusu makundi hayo kuwa wako baadhi ya wabunge ambao pia wamevamia na kuathiriwa mali zao.

Akijibu mwongozo huo, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, aliagiza serikali kushughulikia jambo hilo kwa haraka.

Kuhusu bunge kuahirisha ratiba, Spika alisema jambo hilo kwa masharti ya kanuni ya 55, wao kama wabunge, ni dhahiri wangeweza kulijadili, lakini kwa namna lilivyo na kwa namna kanuni ya 55 ilivyoweka masharti, hilo ni moja ya mambo ambayo yanaangukia katika kifungu cha 3 (3) cha Kanuni ya 55 na kwa masharti ya Kanuni ya 55 (i) (ii), hilo ni jambo ambalo linapaswa kushughulikiwa na serikali katika utaratibu wa kawaida.

"Kwa hiyo litashughulikiwa na serikali kwa utaratibu wa kawaida. Lakini kwa sababu Mheshimiwa Bahati, kwa namna alivyolieleza jambo hili namna ambavyo limeshaathiri maisha ya mtu au watu, limeshaathiri mali za watu na jana (juzi), tulizungumza pia hapa (Bungeni) athari zinaenda mbali zaidi ya hapo.

"Sasa pamoja na kwamba kanuni inasema serikali italishughulikia katika utaratibu wa kawaida, ni kwamba itachukua hatua kama yale mambo mengine yote inavyokuwa hapana!

"Tunaipa fursa serikali ilishughulikie jambo hili kwa haraka. Yaani kanuni inaposema utaratibu wa kawaida ni kwamba ni utaratibu wa kawaida kwa maana ya sheria ile inayoshughulika na mambo haya, inatoa fursa ya serikali kuchukua hatua," alisema.

Spika alisema serikali ina uwezo wa kuchukua hatua kwa kuwa taifa lilishapata hizo changamoto na serikali ilifanyia kazi na hayo mambo yakaisha kabisa, hivyo wanaamini hata hilo inao uwezo wa kulimaliza.

"Kwa sababu zile athari, si tu kwa sababu na wabunge wameathirika, maana wabunge wameathirika mali zao na si kwa maana ya maisha, lakini kimsingi hata maisha yangeweza kuchukuliwa kwa sababu wako walioumizwa na matukio haya.

"Lakini si kwa sababu ni ya wabunge, hata huko nje wananchi wanapata athari. Kwa hiyo serikali ichukue hatua za haraka kushughulikia jambo hili," alisisitiza.

"Serikali naiagiza ichukue utaratibu wake wa kawaida, kwa sababu bado tuko hapa (Bungeni). Tunaamini kwamba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, yuko hapa (George Simbachawene), mtalichukulia jambo hilo kwa uzito unaostahili na kuchukua hatua zile ambazo tunazitarajia kutoka kwenu," aliongeza.

Wakati anasimama kuomba mwongozo huo, Ndingo alisema anaomba Bunge liahirishwe kwa muda ili kujadili jambo la dharura kwa Kanuni ya 54 kwa kuwa linalohusu usalama wa raia.

Akijenga hoja hiyo, mbunge huyo alisema: "Mheshimiwa Spika, tumeendelea kupata taarifa na kuona taarifa mbalimbali jana katika Mkoa wa Dar es Salaam, kuhusiana na Panya Road.

"Wanaendelea na uvamizi kwenye makazi ya watu na barabarani, lakini jana wamesababisha mauti ya raia. Lakini vilevile vikundi kama hivi vimeendelea nchini huko mkoa wa Mara, wanajiita Watu Kazi na wanaendelea na matukio hayo.

Lakini jimboni kwa Mheshimiwa Chaya (Manyoni Mashariki-Singida), Mheshimiwa Diwani amevamiwa.

"Kwa hiyo ni matukio ambayo Mheshimiwa Spika yanaendelea kwa kasi, lakini vilevile hata hapa Dodoma, baadhi ya waheshimiwa wabunge tayari wameshavamiwa na vikundi mbalimbali vya vijana hawa."

Kutokana na uvamizi huo, Mbunge huyo alisema kwa kuwa jambo hilo ni la dharura, anaomba kwa unyeti wake, hivyo Bunge liahirishwe kwa muda ili kulijadili na kuishauri serikali.

Septemba 14, mwaka huu, Polisi Kanda Maalum ya Dar es Saalam, ilithibitisha kuuawa kwa mwanafunzi wa mwaka wa pili wa shahada ya kwanza ya uandishi wa habari katika Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma (SJMC) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Maria Basso (24).

Mwanafunzi huyo, kwa mujibu wa taarifa, alifariki dunia baada ya zaidi ya watu 10 kuvamia nyumbani kwao, Kawe Mzimuni.

Inaelezwa kuwa Maria, alivamiwa na kusababishiwa kifo na wahalifu hao waliokuwa na silaha za jadi, ambao walivamia nyumbani kwa Paschal Basso (56).

Baada ya kuvamia nyumba hiyo yenye vyumba 15, walivunja milango na kupora fedha, simu za mkononi, kujeruhi watu watatu na kumuua Maria Basso.

HABARI KITAIFA

# Washauri kuruhusiwa mgombea binafsi

**Na Sabato Kasika**

WADAU wa demokrasia wameshauri utaratibu wa kuwapo kwa mgombea huru uruhusiwe, kama njia mojawapo ya kupanua demokrasia nchini.

Ushauri huo ulitolewa jijini Dar es Salaam jana na Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Richard Mbunda, katika maadhimisho ya Siku ya Demokrasia Duniani na miaka 30 ya urejeshwaji wa vyama vingi vya siasa nchini.

"Ibara ya 21(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaruhusu kila Mtanzania kushiriki shughuli mbalimbali ikiwamo kugombea nafasi za uongozi katika vyama vya siasa," alisema Dk. Mbunda.

Aliongeza kuwa nchini mfumo unaotumika katika kupata uongozi wa kisiasa ni lazima kupitia chama na kwa hali hiyo inawafanya baadhi ya Watanzania wasio kwenye vyama kukosa nafasi hizo.

"Huo ni ukiritimba tu ambao ingefaa tuachane nao ili kuruhusu mgombea huru kwa nafasi yoyote bila kupitia chama ili kupanua wigo wa demokrasia," alisema.

Alipendekeza Watanzania kupewa uhuru wa kushiriki katika siasa bila kupitia chama, kwa kuwa mfumo huo unarudisha nyuma harakati za kila Mtanzania kushiriki shughuli za maendeleo.

Alisema baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakitumia mwanya huo kuwabana wenzao wakimbie vyama na kuacha wazi nafasi za uwakilishi, kutokana na mfumo kutoa mwanya huo.

Dk. Mbunda alivitaka vyama vya siasa kuwa vya uwakilishi wa maslahi ya umma na sio ya watu wachache, mazingira kama hayo yanaweza kusababisha migogoro ya ndani.

Mbunge wa Ubungo Dar es Salaam, Prof. Kitila Mkumbo aliwataka viongozi wa vyama vya upinzani kudumisha demokrasia ndani ya vyama vyao.

Alisema baadhi ya wadau katika maadhimisho hayo, walionyesha kuilaumu CCM kuwa inachangia kuminyina demokrasia bila kuangalia hali ilivyo ndani ya vyama hivyo.

Kiongozi wa Jumuiya na Taasisi za Kiislam, Sheikh Rajabu Katimba, alishauri kuwapo uwanja sawa kwa vyama vyote vya siasa, ili kuondoa malalamiko kama hayo yaliyojitokeza katika maadhimisho hayo.

Mwenyekiti wa CUF, Prof. Ibrahimu Lipumba, alisema miaka 30 ya urejeshwaji wa vyama vingi vya siasa nchini, upinzani umepitia machungu mengi na kwamba ipo haja ya kufanya mabadiliko.

"Mikutano halali ya kisiasa inazuiwa, lakini angalau sasa kuna uelekeo mzuri hasa baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuunda kikosi kazi, ili kuangalia uwezekano wa kuendesha shughuli za kisiasa," alisema.

# Rais atoa neno mikutano hadhara vyama vya siasa

**Na Samia Suluhu Hassan**



Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA: MAKTABA**

MWAKA 2007, Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa ulifanya uamuzi wa kuzitaka nchi duniani kuadhimisha Siku ya Demokrasia kila ifikapo Septemba 15, ya kila mwaka.

Siku hii inaadhimishwa kwa madhumuni ya kukuza na kuendeleza demokrasia katika kila nchi kwa mifumo inayokubalika. Hivyo, katika siku ya leo, sisi kwa upande wetu kama nchi tunapaswa kuzungumzia yanayoikabili demokrasia yetu.

Katika kuadhimisha siku hii, hakuna budi, ila kuwashukuru Watanzania wote kwa kuendelea kudumisha amani na utulivu nchini. Hapa, niungane na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika ujumbe wake alioutoa leo (jana) kwa dunia kwamba nanukuu: "Sasa ni wakati wa kuhakikisha kwamba Demokrasia, Maendeleo na Haki za Binadamu ni mambo yanayoshikamana. Sasa ni wakati wa kusimama na misingi ya kidemokrasia, ya usawa, ushirikiano na umoja."

Pamoja na kwamba kwa mwaka huu 2022, Umoja wa Mataifa umejielekeza kuzungumzia demokrasia kwa vyombo vya habari na kwa kuwa hakuna mfumo mmoja wa kuendesha demokrasia duniani, kwa upande wetu, tunajielekeza kuzungumzia jambo ambalo limekuwa likidaiwa sana na vyama vya siasa hapa nchini.

Vyama vya siasa vimekuwa vikidai kuruhusiwa kuendelea kufanya kazi za kisiasa, hususan kufanya mikutano ya hadhara na wanachama wao.

Serikali itumie fursa hii kueleza kwamba, Kikosi Kazi kinachoratibu maoni ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa kimeendelea kusisitiza kutolewa kwa ruhusa ya kuendesha mikutano ya vyama vya siasa, ila wameonyesha wasiwasi kwenye sheria na kanuni zinazosimamia suala hilo.

Demokrasia ni mchakato unaohusu namna ya uendeshaji wa mambo kuendana na matakwa ya wananchi kisiasa, kiuchumi, kijamii na kwa kufuata mila na desturi za nchi husika, pamoja na ushirikishwaji wa wananchi.

Tanzania tuko katika hatua mbalimbali za kutanua wigo wa ushirikishwaji wananchi kwa kuzingatia mazingira yetu, huku tukiongozwa na moyo wa maridhiano yanayotujengea usawa, mshikamano na umoja.

Hivyo basi, kwa muktadha huu, nashauri kwamba tusubiri maoni na mapendekezo ya Kikosi Kazi juu ya marekebisho ya sheria na kanuni hizo na kwamba suala hili litatolewa tamko siku chache zijazo.

***Kazi Iendelee!***

# Biashara uuzaji sarafu yashamiri vituoni Dar

**Na Waandishi Wetu**

BIASHARA ya uuzaji wa sarafu maarufu kama 'chenji' katika vituo vya daladala imeendelea kushamiri jijini Dar es Salaam, licha ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT), kuipiga marufuku.

Uchunguzi wa Nipashe katika maeneo mbalimbali jijini Dar es Salaam, umebaini ongezeko la biashara hiyo, huku wafanyabiashara hao wakiifanya kwa uwazi kando ya vituo vya daladala.

Biashara hiyo inahusisha uuzaji wa sarafu kwa mtu kutoa noti ya Sh. 1,000 na kukatwa kati ya Sh. 200, Sh.100 na Sh. 50, huku noti ya Sh. 5,000 ikikatwa Sh. 500 na Sh. 10,000 ni Sh. 1,000 hadi 2,000.

Wanaofanyabiashara hiyo huenda benki na kubadili noti kwenda kwenye sarafu na kisha kuziuza kwa makondakta na madereva wa daladala ambao wana uhitaji mkubwa wanapokuwa kwenye kazi yao ya kurudishia abiria chenji.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wafanyabiashara hao walisema wanauza sarafu kwa bei tofauti kulingana na eneo la kituo husika.

Mmoja wa wafanyabishara hiyo, Ernest Mwitaba, alisema uuzaji wa sarafu na noti unatofautiana kulingana na kituo cha daladala na uhitaji wa huduma hiyo.

"Tunatofautiana katika uuzaji kutegemeana na stendi au sehemu husika, hapa Mbezi, Mwenge na Makumbusho bei ni hiyo hiyo (Sh. 5,000 kwa Sh. 500), lakini Posta bei tofauti wanauza Sh. 5,000 kwa Sh. 700," alisema.

Alisema kwa sasa hana sehemu maalum ya kuweka biashara yake kutokana na katazo la kuuza sarafu kwenye vituo na badala yake anatembeza barabarani kwa siri.

"Tangu mama (Rais) akataze kuweka biashara vituoni tumekuwa tukifanya biashara zetu kwa siri tukizunguka vituoni, wakija mgambo wanatufukuza, tunauza huku macho yako juu juu," aliongeza.

Kwa upande wake, Simon Ndosi, alisema biashara hiyo inamnufaisha na ameamua kuiweka pembezoni mwa kituo cha Mwenge Dar es Salaam.

"Tumeamua kufuata agizo la serikali la kutofanya biashara kwenye vituo vya daladala, tumekuwa tukifanya kwa kuiba iba hapa wakitokea mgambo tunakimbia," alisema Ndosi.

"Biashara hii inatufanya tuendeshe maisha yetu vizuri tu tofauti na mtu kukaa na kufanya vitendo vya uhalifu kama wizi," aliongeza.

"Kusema kweli mamlaka haitambui biashara yetu na kuna kipindi walituambia uuzaji wa chenji kiholela kama hivi sio halali kisheria," alisema.

Madereva na makondakta wa daladala kwa upande wao, walisema biashara hiyo ina changamoto yake kwa sababu husababisha hesabu ya posho yao kupungua wanapomaliza kazi.

Kondakta wa daladala ya Makumbusho-Bunju, Kachua Mrutu, alisema ununuzi wa sarafu huathiri posho yao kwa siku kutokana na kiasi kikubwa cha fedha kubaki kwa wafanyabiashara wa chenji.

"Unafika hapa Makumbusho na Sh. 30,000, lakini Sh. 7,000 inaishia kwa muuza chenji, karibu hela ya abiria watano au kumi inabaki kwake," alisema.

Dereva wa daladala za Makumbusho-Temeke, Shadrack Mrindoko, alisema wanalazimika kununua chenji kutokana na uhitaji mkubwa katika kazi yao.

Meneja Idara ya Sarafu Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Said Ilulu, alithibitisha kuwapo kwa biashara hiyo na kubainisha kuwa sio halali kisheria, huku akiahidi uchunguzi unafanyika na kuchukua hatua.

"Huwezi kuuza fedha ya kitanzania kwa fedha ya kitanzania, tunalifahamu hilo tunaendelea na uchunguzi kisha tutawajulisha baada ya siku kadhaa," alisema Ilulu.

***Imeandikwa na Said Muhibu (SAUT), Golden Kisapile (TUDARCo).***

# Kampuni za kigeni 75 zatafuta fursa uwekezaji

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, amesema zaidi ya mataifa 10, kampuni 75 zimekutanishwa na wawekezaji na wafanyabiashara wazawa nchini ili kutafuta fursa za uwekezaji nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Dk. Kijaji alisema mkutano huo umeandaliwa na Benki ya Dunia (WB), kupitia taasisi yake ya MIGA kwa kushirikiana na serikali.

Alisema lengo la mkutano huo ni kuwaunganisha wawekezaji wazawa kuchangamkia fursa kutoka kwa wenzao.

"Wale wanaolalamika hawana mitaji, tunawaunganisha na kampuni kubwa zenye mitaji, tunawaomba waje wapate mitaji na kufanya kazi kwa pamoja ili tuweze kufanikiwa, mitaji ipo Benki ya Dunia.

"Wafanyabiashara na wawekezaji wetu wa ndani wanakwenda kunufaika kwa kiwango kikubwa, tunachokiangalia ni kwenda kutengeneza ajira za kutosha kupitia uwekezaji huu."

Dk. Kijaji alisema awali walianza na mkutano wa uwekezaji uliohusisha eneo huru la biashara Afrika uliofanyika kwa siku tatu, ukilenga kufungua fursa za biashara kwa wanawake na vijana barani.

Alisema serikali imefanya marekebisho mbalimbali kupitia Sheria ya Fedha mwaka jana kwa kuondoa tozo sumbufu zaidi ya 132.

Kijaji alisema matarajio ya mkutano huo ni kuwakutanisha wawekezaji wakubwa kutoka nje wakutane na wenzao wa hapa nchini ili kuangalia fursa za uwekezaji.

Dk. Kijaji alisema hali ya uwekezaji nchini ni nzuri na kwa mwaka 2021/22, katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), wameandikisha miradi 528 yenye thamani zaidi ya Shilingi trilioni moja.

Kuhusu malori yaliyokwama mpaka wa Tanzania na Kenya eneo la Namanga, alisema serikali inaendelea kushughulikia, akieleza kwamba hakuna lori lililozuiliwa kuingia nchi husika.

"Rais Samia Suluhu Hassan, alipoapishwa mwaka jana, safari yake ya kwanza ilikuwa Kenya. Kazi ya wizara ni kuhakikisha biashara inafanyika kwa kuzingatia sheria. Kinachowakwamisha malori yetu pale mpakani, Waziri wa Kilimo ameshasema, narejea.

"Ni kwamba huko nyuma walizoea kufanya biashara bila kufuata taratibu na sheria, sasa tumerudi kwenye taratibu na sheria, lazima tujue unasafirisha mahindi kiasi gani na ni salama au siyo salama ili Watanzania, lazima tuelewane.

Mtaalamu wa Diplomasia ya Uchumi kutoka Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Raphael Maganga, alisema kupitia mkutano huo, wamenufaika na mambo mawili ambayo ni nchi kufunguka na wawekezaji kuja.

Alisema kwa sasa wawekezaji wanaweza kuwasaidia wenzao wa kutoka nje kuja kuwekeza nchini na kupata uhakika wa mitaji yao.

Kuhusu kero, Maganga alisema walikuwa nazo mbili mojawapo ni ukosefu wa mitaji na kwamba kupitia mkutano huo wameanza kuona fursa.



Meneja wa Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Mhandisi Joanes Martin (kulia), akikabidhiwa zawadi ya mbuzi, baada ya Serikali kufanikisha mradi wa maji utakaonufaisha wakazi 2,204 wa Kijiji cha Losoito, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Auawa kwa kukatwa shingo akiwa lindoni

**Na Samson Chacha,** TARIME

MWENYEKITI wa Kitongoji cha Nyatiti, Kijiji cha Buriba Kata ya Sirari, wilayani Tarime, mkoani Mara, Alex Marwa (40), ameuawa na watu wasiojulikana kwa kukatwa shingo akiwa katika lindo lake la tangi la maji.

Wakizungumza na mwandishi wa gazeti hili, kaka wa marehemu, Joseph Marwa, Ofisa Idara ya Maji, Kata ya Sirari, Musa Lameck na Ofisa Mtendaji wa Kata ya Sirari, Wakuru Mirumbe, walisema Alex alipatwa na umauti huo usiku wakati akiwa katika lindo lake la mashine na tangi linalosambaza maji katika kata za Sirari na Gwitiryo, kwa kukatwa mapanga shingoni na kuning'inia hali iliyosababisha kifo chake papo hapo.

Walisema mwili wa marehemu ulikutwa alfajiri na Ofisa Idara ya Maji nje ya mlango wa chumba cha mashine alipokwenda kumwona mlinzi huyo ili awashe mashine ya kusukuma maji.

Alisema alimkuta amelala chini akiwa tayari ameshafariki akiwa na majeraha makubwa ya kukatwa shingo.

Alisema alitoa taarifa kwa ndugu zake, viongozi wa serikali na Polisi ambao walifika kuuchukua mwili na kuupeleka kituo cha afya kwa uchunguzi zaidi.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Tarime Rorya, ACP Geofrey Sarakikya, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

Hilo ni tukio la pili la mauaji jirani na kitongoji hicho katika kipindi cha wiki tatu. Mkazi wa Kitongoji cha Buhemba Kijiji cha Ng'ereng'ere, Matinde Masaite aliuawa kwa kukatwa shingo na katika tukio hilo watu wawili wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma hizo.

# CAG Zanzibar aonesha mil. 700/- zilivyoliwa

**Na Mary Geofrey**

RIPOTI ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Zanzibar, imebaini kuwapo ubadhirifu wa zaidi ya Sh. milioni 700 za Mradi wa Hifadhi ya Eneo la Kihistoria la Mkamandume, unaotekelezwa na serikali kwa Sh. bilioni 1.4.

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Zanzibar iliingia mkataba na kampuni ya Shamjo, kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha utoaji huduma pamoja na ukarabati wa maeneo ya historia ya Mkamandume, kwa gharama hizo ambazo zimetolewa na serikali kwa asilimia 100.

Malengo ya mradi huo ni kuifanya Zanzibar inufaike zaidi kiuchumi bila ya kuharibu mila na utamaduni wa asili na kuhakikisha mazingira ya Zanzibar yanabaki salama pamoja na kuimarika kwa huduma za utalii.

Malengo mengine ni kuifanya Zanzibar iwe ni kituo bora zaidi kwa watalii wa daraja la juu na kusimamia utalii ili kuweza kukua pamoja na kupanga mipango madhubuti ya kuimarisha huduma za utalii.

Kupitia ripoti ya ukaguzi wa fedha za serikali ya Juni mwaka 2021 ya CAG, Dk. Othman Abbas Ali, alionyesha kuwapo kwa ubadhirifu huo ambao ulichangiwa na kasoro mbalimbali walizobaini.

Alisema katika ripoti hiyo, walibaini kutokuwapo na daftari la kuhifadhia kumbukumbu licha ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba kumiliki mali mbalimbali za kudumu yakiwamo maeneo ya kihistoria katika kisiwa cha Pemba.

Alisema kukosekana kwa kumbukumbu hizo ni kushindwa kuthibitisha uwapo na uhifadhi wa maeneo ya kihistoria katika kisiwa cha Pemba na kuwa kinyume cha kifungu namba 29 (2) cha sheria namba 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Dosari nyingine ni kukosekana kwa vielelezo vya Sh. milioni 56 ambazo zimelipwa kwa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kwa ajili ya ulipaji wa kodi ya ongezeko la thamani VAT inayotokana na ujenzi wa kituo cha utoaji wa huduma katika eneo la kihistoria Mkamandume.

Kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba na Bill of Quantity (BOQ), malipo ya kodi ya asilimia 18 ya VAT ilikuwa ni Sh. milioni 56 ya gharama zote za ujenzi wa Sh. milioni 311.4 za gharama ya ujenzi.

Aidha, ripoti ilionyesha kuwa, ukaguzi uliofanyika ulibaini kuwa, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba ilifanya malipo ya Sh. milioni 30.2 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbalimbali vya ujenzi wa kituo cha kutolea huduma kilichojengwa katika eneo la Mkamandume lakini manunuzi ya vifaa hivyo hayakuzingatia thamani halisi kwa wakati huo na imebainika kwamba vifaa hivyo vingeweza kununuliwa kwa jumla ya Sh. milioni 15.1.

CAG pia alibaini kuwapo kwa manunuzi ya vifaa vya Sh. milioni 15.1 ambavyo vilikusudiwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kituo cha utoaji wa huduma katika eneo la kihistoria la Mkamandume lakini vifaa hivyo havikuonekana kwa ajili ya ukaguzi.

Alitaja dosari nyingine kuwa ni Sh. 116.6 zilitumika kwa ajili ya ukarabati wa Kisima cha Wivu katika eneo la kihistoria la Mkamandume ili kuboresha muonekana mzuri na halisi wa kisima lakini dosari iliyobainika ni kwamba thamani halisi ya fedha zilizotumika katika ukarabati wa kisima hicho hailingani na hali halisi.

Alisema katika kufanya ufuatiliaji wa ukarabati huo imebainika kwamba gharama zilizotumika ni kubwa na hivyo kutokuendana na thamani halisi ya ukarabati uliofanyika kwa kutokuzingatiwa kwa hali ya uchumi, ufanisi wa kazi iliyokusudiwa pamoja na malengo halisi yaliyopangwa katika utekelezaji wa mradi huo.

# CRDB yapata mabilioni kuwezesha biashara

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imeingia mkataba wa makubaliano na Benki ya Kimataifa ya Intesa Sanapaolo ya Italia na Benki ya Investec ya Afrika Kusini unaoiwezesha CRDB kupata dola za Marekani milioni 130 kwa ajili ya kukopesha sekta za biashara na wajasiriamali nchini.

Mapema mwaka huu, CRDB iliingia mkataba wa awali na benki hizo za kimataifa kusaidia kupatikana fedha katika masoko ya kimataifa kwa ajili ya kuimarisha mtaji wa benki hiyo na kukuza uwezo wa kutoa mikopo.

"Tunafurahia sana kufanikisha makubaliano haya. Fedha hizi zilizopatikana kutoka masoko ya kimataifa, zitasaidia kuimarisha mtaji wa benki yetu na kukuza uwezo wetu wa kutoa mikopo kwa wateja wakubwa na wadogo hapa Tanzania na Burundi.

"Kipekee niwashukuru Investec Bank na Intesa Sanpaolo kwa ushirikiano waliotupa," alisema Abdulmajid Nsekela, Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB wakati wa kutia saini makubaliano hayo jijini Dar es Salaam jana.

CRDB inakuwa benki ya kwanza nchini kupata fedha za uwekezaji kutoka masoko ya kimataifa. Kwa mujibu wa Nsekela, lengo lilikuwa ni kukusanya dola milioni 50, lakini viwango bora na ufanisi mkubwa wa benki hiyo ulivutia wawekezaji wengi wa kimataifa na kupelekea kupatikana kwa dola milioni 130.

Nsekela alisema CRDB ni moja ya benki 10 zilizoorodheshwa kama benki bora na salama zaidi kuwekeza barani Afrika na Moody`s Investors Services na kupewa daraja la 'B1 Outlook' ambalo ni daraja la juu zaidi kwa taasisi za fedha katika ukanda wa Jangwa la Sahara. Mwaka huu benki hiyo pia imetajwa kuwa 'Benki Bora Tanzania' na jarida maarufu la Uingereza.

"Kama benki inayoongoza nchini Tanzania, CRDB inaendelea kutazama fursa za biashara katika sekta za kimkakati ili kukuza uchumi wa nchi. Fedha hizi zitatusaidia kuimarisha shughuli zetu za utoaji mikopo hususani mikopo ya wanawake na vijana na kuimarisha zaidi nafasi yetu katika soko kama benki inayoongoza kwa kufadhili sekta za uchumi," alisema Nsekela.

Rowan King, Mkuu wa Usuluhishi wa Mikopo kwa Afrika kutoka Benki ya Investec, alisema kupatikana kwa fedha hizo katika masoko ya kimataifa kunaonyesha imani ya taasisi za fedha duniani kwa Benki ya CRDB na uchumi wa Tanzania.

"Tanzania imeonekana kuwa sehemu muhimu ya hadithi ya ukuaji wa Afrika katika miaka michache iliyopita. Bidhaa nyingi muhimu zinazozalishwa Afrika Mashariki, zinasafirishwa nje ya nchi kupitia bandari za Tanzania. Tanzania ina jukumu muhimu katika biashara katika kuimarisha biashara baina ya nchi za Afrika," alisema.

Gustaaf Eerenstein, Mkurugenzi wa Huduma za Mikopo ya Pamoja Benki ya Investec, alisema: "Dola milioni 130 zilizopatikana ni mara mbili na nusu ya kiasi kilichokusudiwa. Hii inaonyesha kiwango cha juu cha imani ambayo wawekezaji wanayo kwa Benki ya CRDB."

Ushirikiano huo na CRDB na benki za Intesa Sanpaolo na Investec unaendelea kuimarisha uwezo wa CRDB katika kutoa mikopo, ambapo mwaka huu pekee imeingia makubaliano ya zaidi ya Dola za Marekani milioni 300 na mashirika kama IFC, AFDB, AGF, PROPARCO, USAID na DFC kwa ajili ya uwezeshaji wa biashara ndogo na za kati (SME) na uwezeshaji wa kiuchumi kwa wanawake na sekta zisizo rasmi.

# Serikali yakiri tatizo kupata vitambulisho vya NIDA

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, amekiri kuwapo kwa tatizo la upatikanaji wa Vitambulisho vya Taifa (NIDA), kutokana na mkataba wa mkandarasi aliyekuwa akitoa huduma hiyo.

Tatizo lingine ni upungufu wa kadi ghafi na upatikanaji wake kwenye soko la dunia kutokana na athari za UVIKO-19.

Masauni aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fakharia Shomari.

Mbunge huyo alisema kumekuwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa vitambulisho hivyo na kutaka waziri aseme njia gani rahisi ambayo wananchi wanaweza kuvipata bila usumbufu.

"Vitambulisho vya NIDA ni kazi kubwa kuvipata na ni janga kubwa, je, waziri atatuambia vipi taifa njia ya kupatikana kwa urahisi na wapite njia gani kwasababu ni haki yao?" Alihoji.

Waziri Masauni alijibu kuwa matatizo hayo yalisababisha kutokuwapo kwa kadi za kutosha kuzalisha vitambulisho hivyo na serikali imefanya jitihada kuhakikisha yanatatuliwa.

"Nitoe wito kwa wananchi kwamba upatikanaji wa namba ya kitambulisho unaweza kuwafanya kupata huduma mbalimbali za kijamii, kwa wale wanaosubiri kupata kadi zao waendelee kutumia namba za utambulisho wakati serikali ikiendelea na jitihada za kuhakikisha wanapata vitambulisho," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Momba, Condester Sichalwe, alisema ndani ya jimbo hilo kuna watu wameshindwa kuandikishwa Mfuko wa Tasaf na kupata mbolea ya ruzuku kutokana na kutokuwa na vitambulisho hivyo.

Waziri Masauni akijibu, alisema namba za utambulisho zinaweza kutumika kupata huduma mbalimbali.

Alisema kwa mwaka huu wa fedha serikali imetenga Sh. bilioni 42.5 kwa ajili ya ununuzi wa kadi ghafi milioni 8.5.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Ngorongoro (CCM), Emmanuel Shangai, alihoji ni lini serikali itawapatia vitambulisho vya taifa na vyeti vya kuzaliwa wananchi wa Kata za Ololosokwan, Soitsambu na Enguserosambu Ngorongoro.

Masauni alijibu hadi kufikia mwezi Agosti 2022 jumla ya wananchi 84,637 katika Wilaya ya Ngorongoro wametambuliwa na kusajiliwa.

Alisema namba za utambulisho 61,237 sawa na asilimia 72.3 ya wananchi wote waliotambuliwa na kusajiliwa zimezalishwa na kugawiwa kwa wananchi na kuwa jumla ya vitambulisho 46,997 sawa na asilimia 76.7 vimezalishwa na kugawiwa kwa wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro.

Masauni alisema usajili na utambuzi wa wananchi na uzalishaji na ugawaji vitambulisho vya taifa ni kazi endelevu na kuwa mamlaka itaendelea na usajili wa wananchi wanaokidhi vigezo kupitia ofisi za usajili za wilaya pamoja na kuzalisha na kugawa vitambulisho vya taifa kwa wananchi kupitia katika kata zote.

Alisema usajili na utoaji wa vyeti vya kuzaliwa bila malipo unaendelea katika vituo vyote vinavyotoa huduma ya afya ya mama na mtoto pamoja na vituo vya kata.




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akiweka jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa chanzo na kituo kipya cha kusafisha na kutibu maji Butimba, mkoani Mwanza juzi, utakaogharimu Sh. bilioni 69 unaotarajia kuwanufaisha wananchi 450,000. **PICHA: NEEMA EMMANUEL.**

# Philip Mpango akemea urasimu huduma za maji

**Na Vitus Audax,**
MWANZA

MAKAMU wa Rais Dk. Philipo Mpango ametaka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) kuacha urasimu wa kuchelewesha kuwaunganishia wananchi maji na kuwabambikizia bili mwisho wa mwezi.

Dk. Mpango alisema hayo juzi baada ya kuweka jiwe la msingi katika mradi wa ujenzi wa chanzo na kituo cha tiba ya maji cha Butimba jijini Mwanza.

Alisema tabia hiyo inawaumiza wananchi wa kawaida wanaohitaji huduma hiyo na kwamba lazima MWAUWASA wahakikishe wanaipiga vita na kuimaliza.

Dk. Mpango pia aliagiza kuwa suala la kuunganishiwa maji linatakiwa lisizidi siku saba na kuwataka maofisa idara ya maji mkoani Mwanza kuacha tabia za urasimu na kuwabambikizia bili wananchi.

Alisema bado kuna tatizo la upatikanaji wa maji licha ya mkoa huo kuwa na chanzo cha maji ambacho ni Ziwa Viktoria na kuitaka Wizara ya Maji kuhakikisha wanaongeza juhudi katika ujenzi wa mradi huo ili kupunguza kero hiyo kwa wananchi.

"Hakikisheni mnaongeza kiwango cha usambazaji wa maji katika kituo hiki, simamieni mradi huu usiku na mchana ili ukamilike kabla ya mwishoni mwa mwaka huu na itanibidi kula siku kuu ya krismasi hapa Mwanza ili nihakikishe huu mradi umekamilika," alisema Dk. Mpango.

Naye Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema wizara yake imepokea maelekezo hayo na itahakikisha wanakamilisha mradi huo ifikapo Desemba kama alivyoagiza. "Tayari tumeongea na mkandarasi na kutuhakikishia kuwa mradi huu utakamilika mwishoni mwa mwezi wa 12 mwaka huu badala ya mwezi wa pili kama ilivyokuwa katika tathmini ya mradi huu," alisema Aweso.

Awali akizungumza katika hafla hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, alisema kuwa kwa sasa mkoa huo una idadi kubwa ya watu ikilinganishwa na kasi ya usambazaji wa maji iliyopo.

Malima aliomba Wizara ya Maji kuongeza wigo wa miradi ya usambazaji wa maji mkoani humo ili wananchi wapate huduma iyo bila usumbufu.

Mradi huo wa maji wenye thamani ya Sh. bilioni 69 unatarajiwa kutatua kero za maji katika maeneo ya pembezoni mwa jiji la Mwanza pamoja na baadhi ya wilaya mkoani Mwanza.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# 'Panya road' wanaweza kudhibitiwa

**MAKUNDI** ya panya road yanayoendelea kutishia maisha na usalama wa raia na mali zao yanaweza kudhibitiwa kama kutakuwa na nguvu ya pamoja.

Makundi hayo yanapoachiwa kuendelea kunyanyasa raia kwa kunyang'anya mali zao, kujeruhi na kufikia hatua mpaka ya kuua ni dalili mbaya na mnyororo wa matukio hayo utaendelea kukua.

Ni matukio mfululizo yametokea siku za hivi karibuni kwa makundi hayo kuvamia nyumba za watu, kufunga mitaa na kunyang'anya mali za watu.

Matukio hayo yanasababisha wananchi kuishi maisha ya hofu kwa sababu wakati mwingine yanatokea mchana kweupe.

Makundi ya panya road mengi yanaongozwa na vijana wadogo ambao hubeba silaha za jadi kama mapanga, visu na bisibisi na hufanya matukio ya uvamizi bila huruma.

Tumeona Bunge limeamua kulivalia njuga suala hilo kwa kuitaka serikali kuchukua hatua za haraka na kwa uzito unaostahili, kuyakabili na kuyadhibiti makundi hayo ya kihalifu.

Hatua hiyo imetokana na baadhi ya wabunge, kuomba Bunge kuahirishwa na kujadili jambo la dharura, ambalo ni kukithiri kwa uhalifu unaofanywa na vikundi hivyo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mara na Singida.

Imeelezwa kuwa kuna wabunge tayari wamevamiwa na makundi hayo na kuathiriwa mali zao.

Jana, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, aliiagiza serikali kushughulikia jambo hilo kwa haraka, wakati alipokuwa akijibu mwongozo ulioombwa na wabunge wawili, Bahati Ndingo (Viti Maalum-CCM) na Mbunge wa Segerea (CCM), Bonna Kamoli.

Spika Dk. Tulia, alisema serikali ina uwezo wa kuchukua hatua kwa kuwa taifa lilishapata hizo changamoto na ilifanyia kazi na hayo mambo yakaisha kabisa. Hivyo, wanaamini hata hilo inao uwezo wa kulimaliza.

Hata hivyo, Spika Tulia amezungumzia hatua hiyo haitokani kwa sababu wabunge wameathirika, lakini kimsingi hata maisha yangeweza kuchukuliwa kutokana na kuwapo kwa walioumizwa na matukio hayo.

Spika alisema hata huko nje wananchi wanapata athari na kuitaka serikali ichukue hatua za haraka kushughulikia jambo hilo.

Wakati anasimama kuomba mwongozo huo, Mbunge wa Viti Maalum, Bahati Ndingo, alisema anaomba Bunge liahirishwe kwa muda ili kujadili jambo la dharura, kwa Kanuni ya 54, linalohusu suala zima la usalama wa raia.

Wabunge waliojenga hoja hiyo waliliambia Bunge kuwapo kwa taarifa mbalimbali katika Mkoa wa Dar es Salaam, kuhusiana na Panya road.

Panya road hao wamekuwa wakiendelea na uvamizi kwenye makazi ya watu na barabarani na juzi kusababisha mauti ya raia.

Hoja ya wabunge hao ni vikundi kama hivyo kuendelea nchini katika mikoa mingine kama Mara, wanajiita 'Watu Kazi' na wanaendelea na matukio hayo.

Wabunge hao waliomba kwa kuwa jambo hilo ni la dharura, unyeti wake, Bunge liahirishwe kwa muda waweze kulijadili na kuishauri serikali.

Juzi mwanafunzi mmoja anadaiwa kufariki dunia, baada ya watu zaidi ya 10 kuvamia nyumbani kwao, Kawe Mzimuni.

Mwanafunzi huyo alivamiwa na kusababishiwa kifo chake na wahalifu hao waliokuwa na silaha za jadi.

Kundi hilo la panya road lilivamia nyumba yenye vyumba 15 na kuvunja milango, kupora fedha, simu za mkononi, kujeruhi watu watatu na kumuua mtu mmoja.

Ni matumaini yetu kuwa suala hili kwa kuwa limefika bungeni, litapatiwa ufumbuzi ili liweze kukomeshwa na watu waishi kwa amani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Pilly Kigome

# Ni wakati sahihi, elimu lishe kupamba moto kufuta shida udumavo na damu

**WAKATI** tulikuwa masomoni katika umri mdogo tulifunzwa mengi kuhusu afya ya binadamu. Eneo mojawapo ambalo tulikaririshwa na kueleweshwa ni kuhusu mlo na aina ya vyakula kwamba vipo vya aina tatu; vinavyojenga mwili, kuulinda na mwisho kingine kinachotia nguvu mwilini.

Ni elimu iliyoenda sambamba na kampeni za kupeleka watoto masomoni shule.Naam! Ilikuwa sehemu ya mikakati ya maendeleo, baada ya kupatikana uhuru wa nchi, nasi tukiwa ndiyo bado wadogo sana.

Mitaala ya shule ilienda sambamba nasi, somo la Sayansi Kimu lilitunoa kuzingatia afya yetu, basi ndani yake elimu lishe na ya kujijali ikaenda sambamba kuwa sehemu ya maisha yetu

Tumekuwa wakubwa hata tukatua kliniki, nako tukakuta nadharia hiyo hiyo na masomo yake. Tuliohudhuria hapo, miongoni mwa mambo nyeti tukajifunza ni lishe bora kwa mama, mtoto na familia.

Hata kwenye burudani nje ya kliniki na shule, nakumbuka mwanamuziki maarufu Mbaraka Mwinshehe Mwaruka alishawahi kutunga wimbo maalum wa muziki, akiainisha aina ya vyakula muhimu makundi matatu, ambazo zimeanishwa juu. Pia, ndio ilikuwa sehemu ya sera ya taifa.

Hivyo kwa ujumla wake, ndio inapoibua umuhimu mkubwa wa kutoa elimu ya lishe ngazi ya jamii kote nchini, ili jamii hiyo iweze kujitambua ipasavyo na hata kushiriki kupunguza, kama sio kuondoa magonjwa yanayoweza kupatikana kuhusiana na tatizo la lishe duni.Nikiri katika kizazi hicho tuliona mabadiliko.

**Hivyo kwa ujumla wake, ndio inapoibua umuhimu mkubwa wa kutoa elimu ya lishe ngazi ya jamii kote nchini, ili jamii hiyo iweze kujitambua ipasavyo na hata kushiriki kupunguza, kama sio kuondoa magonjwa yanayoweza kupatikana kuhusiana na tatizo la lishe duni.**

Hivi sasa nimesikia namna malalamiko ya kitaifa kwa asimilia kubwa lishe duni au isiyo na mpangilio sahihi, unaangukia katika kuwaweka watoto wadogo katika kilio cha shida ya udumavu.

Mikoa kama Dar es Salaam na Shinyanga, hivi sasa iko katika orodha ya vinara wa udumavu ambao chanzo kikuu ni lishe duni. Vivyo hivyo, inasikitisha katika baadhi ya mikoa mingine kama Mbeya inataabika kwa udumavu, wakati wana utajiri wa vyakula. Huwa najiuliza shida ni nini?

Hapo linanijia jibu la kwanza elimu na hoja kwamba, sasa ni wakati wetu kujihadhari kuanza kutoa elimu ya lishe kila mmoja kwa nafasi yake na aelimishe na aendeleze, ili jamii iweze kujitambua kuhusiana na ulaji vyakula kwa usahihi kukabiliana na magonjwa yanayoepukika.

Tatizo la upungufu wa damu linaonekana kuwa kubwa katika jamii na moja ya sababu ni ukosefu wa virutubisho lishe muhimu katika mlo.

Ipo sababu kwa serikali kutoa elimu kwa jamii zaidi ya mahali tuliko sasa. Iwe kuanzia ngazi ya kata hadi taifa kwa ujumla, ili wananchi waweze kujitambua na kuanza kukabiliana na tatizo hili.

Kutoka kwa jamii, najua kuna shida ya mwamko wa ulaji wa vyakula na makundi yake. Wapo ambao wanakiri kwa baadhi ya makundi ya vyakula na kusahau ulaji unaoleta virutubisho mwilini.

Ushuhuda wa jamii unaothibitika, unaonyesha wengi wao hawana mwamko wa elimu ya lishe kwa ujumla katika upande wa afya na kuchunguza makundi ya vyakula kwa usahihi na umuhimu na kazi zake mwilini.

Naamini, jamii ikijitambua kikamilifu juu ya umuhimu wa lishe, ni wazi itaweza kupunguza wimbi la tatizo la upungufu wa damu ambalo kwa kiasi kikubwa linatokana na tatizo la lishe duni.

## Sababu kukithiri ukatili, mauaji bayana

**Na Gwamaka Alipipi**

WAKATI vitendo vya ukatili vikiendelea kushika kasi nchini, imeelezwa chanzo kikuu ni tatizo la afya ya akili ambalo linawasibu watu wengi.

Pia wivu wa mapenzi umeelezwa kuwa unachangia kutokea kwa matukio hayo, pamoja na watoto kuonyeshwa ama kufundishwa vitu visivyoendana na umri wao.

Kamishna wa Ustawi wa Jamii kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Nandera Mhando, alibainisha hayo juzi wakati wa Kongamano la Kisayansi, Matatizo ya Ukatili na Uhusiano wa Afya ya Akili, lilioandaliwa na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS).

"Kwa mwaka jana matukio ya ukatili kwa wanawake yalikuwa juu sana asilimia 76, hata ukatili dhidi ya watoto, mikoa ya kanda ya ziwa ndiyo iliongoza kuwa na matukio ya ukatili wa kijinsia, mikoa ya Manyara, Arusha na Dar es Salaam iliongoza kuwa na matukio ya ukatili dhidi ya watoto," alisema.

Dk. Mhando alisema watoto wengi waliopo katika mahabusu wanakabiliwa na kesi za ubakaji, kwamba wengi wao wamefanya vitendo hivyo kutokana na malezi mabaya kutoka kwa wazazi wao.

"Wazazi siku hizi hawalei watoto, wanawapeleka kwa bibi au babu, wengine wanawaachia wasaidizi wa kazi nyumbani, mtoto anapata malezi mabaya tangu akiwa mdogo, mwisho wa siku anafanya matukio ya ukatili," alisema.

Msaikolojia Tiba kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Alex Ndagabwene, alisema: "Tunakutana na watu wengi wengine wana matatizo ya afya ya akili. Chanzo kikuu cha tatizo la afya ya akili ni uvutaji wa sigara, unywaji pombe, uvutaji bangi."

Alisema waathirika hao wanapowapokea huwatibia kwa kuwapatia dawa au saikolojia, kwamba dalili mojawapo ya mtu mwenye tatizo la afya ya akili ni anakuwa na hofu iliyopitiliza, mapigo ya moyo kwenda kasi sana lakini akienda kupima hana tatizo la moyo, anakuwa na wasiwasi mkubwa.

Mhadhiri na Daktari Bingwa wa Afya, Magonjwa ya Akili MNH, Samwel Likindikoki, alisema: "Ukatili dhidi ya wanawake na watoto unasababishwa na tatizo la afya ya akili. Kwa miaka ya hivi karibuni matukio hayo yameshika kasi".

Alisema kati ya watoto 10, saba wanafanyiwa vitendo vya ukatili, watoto wenye umri kati ya miaka mitatu hadi 10 wanabakwa.

Makamu Mkuu wa MUHAS, Prof. Bruno Sunguya, alisema utafiti ambao wamekuwa wakifanya zimekuwa zikileta mabadiliko makubwa, zimesaidia kuboresha sera za kimataifa.

Alisema matukio ya ukatili, afya ya akili bado yanaendelea kutokea nchini, hivyo wananchi wanapaswa kuungana kupiga vita.



Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga (wa pili kushoto), na Mkurugenzi Mkaazi wa Shirika la Chakula Duniani (WFP) Sarah Gordon-Gibson, wakionyesha kabrasha baada ya kutiliana saini makubaliano ya utekelezaji wa mradi wa lishe mashuleni, katika hafla iliyofanyika kwenye shule ya mfano ya Mtemi Mazengo, jijini Dodoma jana. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Saini ya Zumaridi yaibua utata kortini

**Na Pelusy Mihayo,** SAUT

SAINI inayodaiwa kuwa ya Diana Bundala maarufu Mfalme Zumaridi, jana ilizua utata katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza, baada ya kudaiwa imeghushiwa na askari aliyechukua maelezo ya onyo.

Askari huyo ambaye ni shahidi wa upande wa mashtaka katika kesi inayomkabili Zumaridi na wenzake 84, Joseph Robert, amedaiwa kughushi saini ya Zumaridi ambaye ni mshtakiwa namba moja.

Shahidi huyo anadaiwa kughushi saini katika kielelezo cha maelezo ya onyo kilichofikishwa mahakamani kwa ajili ya kutumiwa kama sehemu ya ushahidi mbele ya kesi hiyo inayosikilizwa na Hakimu Mkazi Crescensia Mushi.

Alidai kuwa mshtakiwa namba moja alikiri makosa yake katika kituo cha polisi na kutia saini katika maelezo ya onyo kituoni hapo na kuomba maelezo hayo yapokewe na mahakama kama kielelezo na sehemu ya ushahidi wa kesi hiyo.

Hata hivyo, Wakili wa Utetezi, Erick Mutta, alipinga maelezo hayo kutumika kama kielelezo katika kesi hiyo, huku akidai kuwa aliyetia saini katika maelezo hayo si mshtakiwa bali saini yake imeghushiwa.

Wakili Mutta alidai kuwa mshtakiwa alipigwa kabla ya kuchukuliwa maelezo na kuongeza kuwa maelezo hayo yalichukuliwa nje ya muda kwa kuwa yalichukuliwa dakika 30 kabla, hivyo aliiomba mahakama kulinganisha saini ya mshtakiwa iliyoko katika maelezo hayo na ile iliyopo katika vitambulisho vyake.

Wakili Mutta pia aliiomba mahakama kuweka madai hayo katika maandishi ya kimahakama ili kusaidia katika uamuzi.

Wakili wa upande wa mashtaka, Dorcas Akyoo, alipinga ombi hilo na kudai kuwa saini za mtu zinaweza kuwa zaidi ya moja, hivyo kuomba aulizwe mhusika ambaye ni mshtakiwa kwa kuwa alikuwapo mahakamani.

Mshtakiwa huyo alipoulizwa na mawakili wake juu ya maelezo hayo, alidai kuwa saini hiyo si yake bali imeghushiwa.

Kutokana na utata huo, Hakimu Mushi aliahirisha kesi hiyo hadi Septemba 19, mwaka huu, huku akiutaka upande wa utetezi kuleta ushahidi na vielelezo vitakavyobainisha ukweli wa madai hayo.

# Waziri ataka mpango matumizi ya ardhi eneo la mradi wa maji

**Na Munir Shemweta,** MWANZA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameiagiza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) kuweka mpango wa matumizi ya ardhi katika eneo la mradi wa chanzo na Kituo cha Tiba ya Maji cha Butimba mkoani Mwanza.

Dk. Mabula alitoa wito huo juzi wakati wa uwekaji jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa chanzo na kituo cha tiba ya maji uliofanywa na Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango.

Aliishukuru MWAUWASA kwa kuweka uzio katika eneo linalozunguka mradi huo na kueleza kuwa eneo hilo likiachwa wazi, watu wataingia na ndipo migogoro ya ardhi inapoanza na kusisitiza kuwa mamlaka hiyo imefanya jambo zuri la kuweka uzio.

Waziri alisema pamoja na hatua ya kuwekwa uzio, mpango wa matumizi bora ya ardhi kwenye eneo hilo ni muhimu ili kujua mahitaji ya huduma mbalimbali.

"Chanzo tunakiona kipo lakini wakiweka mpango wa matumizi mazuri kwenye eneo walilozungushia uzio tutajua tuna uhaba wa nyumba za watumishi zinazoweza kuwapo katika eneo hili na wakazi wake wakawa ni sehemu ya walinzi wa mradi.

Uwapo wao utakuwa si tu umeboresha ya maeneo bali tutakuwa tumewapa makazi bora watumishi," alisema.

Kuhusu utunzaji mazingira, Waziri Mabula alisema wizara yake imeelekeza kwamba kwa sasa kila hati inapotoka basi iwe na masharti ya upandaji miti kwa lengo la kutunza mazingira.

Akizundua mradi huo, Dk. Mpango aliagiza mradi huo kukamilika ifikapo Desemba ili iwe zawadi ya Krismasi kwa wakazi wa Jiji la Mwanza na kusisitiza wananchi wanaoishi eneo linalozunguka mradi lazima wapewe kipaumbele katika kupatiwa huduma ya maji.

# Minada vitalu kielektroniki yaingiza mabilioni TAWA

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), imesema ugawaji wa vitalu vya uwindaji wa kitalii kwa njia ya kielektroniki umekuwa wa mafanikio na umeiingizia serikali mapato makubwa.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Kaimu Kamishna wa Uhifadhi wa TAWA, Mabula Nyanda, wakati akizungumza na waandishi wa habari na wahariri kuhusu mafanikio ya mamlaka hiyo.

Alisema utaratibu huo ambao ulianzishwa mwaka 2019 umeleta tija kubwa kwenye biashara hiyo na kwamba umekuwa ukitumika kwenye mataifa mbalimbali duniani kama vile Zimbabwe, Zambia na Namibia.

"Njia hii ya kugawa vitalu vya uwindaji wa kitalii inatoa fursa kwa kampuni za uwindaji wa kitalii kutoka ndani na nje ya nchi kushiriki na utaratibu huu ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 ya CCM inayolenga kuongeza idadi ya watalii hadi milioni tano na mapato hadi Dola za Marekani bilioni sita ifikapo mwaka 2025," alisema Mabula.

Alisema ugawaji wa vitalu vya uwindaji kwa njia ya mnada umesaidia kutoa fursa sawa kwa kampuni yoyote yenye sifa kupata kitalu cha uwindaji kwa njia ya mnada na kuruhusu ushindani kwa kutoa nafasi ya wadau wengi kushiriki ikilinganishwa na utaratibu uliokuwa ukitumika awali.

Mabula alisema utaratibu huo umesaidia kuongeza uwazi na uwajibikaji katika zoezi la ugawaji wa vitalu vya uwindaji wa kitalii ili kuongeza ufanisi katika tasnia hiyo pamoja na kuwezesha kugawiwa kwa vitalu vilivyorejeshwa kwa maudhui ya kutofaa katika uwindaji wa kitalii.

Alisema utaratibu huo umeleta faida ya ongezeko la ada ya vitalu kwa wastani wa asilimia 174 ambapo ada ya kitalu cha daraja la kwanza imeongezeka kutoka dola za Marekani 60,000 na kuuzwa kati ya dola za Marekani 151,000 hadi 285,000.

Mabula alisema ada ya kitalu cha daraja la II imeongezeka kutoka dola za Marekani 30,000 na kuuzwa kati ya dola za Marekani 81,000 hadi 250,000 na ada ya kitalu cha daraja la III kutoka dola za Marekani 18,000 na kuuzwa kati ya dola za Marekani 31,000 hadi 255,000.

Alisema utaratibu huo umesababisha kuongezeka kwa ushindani katika soko kwa vitalu vya uwindaji wa kitalii kwa kuzingatia ubora na daraja la kitalu.

Mabula alisema Mamlaka iliandaa mwongozo wa ugawaji wa vitalu vya uwindaji wa kitalii kwa njia ya mnada Guidelines for Allocation of Hunting Blocks through Auctioning pamoja na mfumo wa kielektroniki wa kufanikisha ugawaji wa vitalu hivyo.

"Tangu kuanza kwa ugawaji wa vitalu kwa njia ya mnada mwaka 2019, TAWA imeendesha jumla ya minada saba ya vitalu vya uwindaji iliyohusisha vitalu 100 hadi kufikia Machi, 2022 na katika awamu zote saba ambazo mnada ulifanyika, vitalu 79 kati ya 100 viliuzwa kwa kiasi cha Dola za Marekani 9,798,000," alisema.

Nyanda alisema kiasi hicho cha fedha ni kikubwa kuliko fedha ambayo ingepatikana kwa kuuza vitalu vyote 79 kwa njia ya kiutawala ambapo zingepatikana Dola za Marekani 3,306,000 sawa na ongezeko la asilimia 196.4.

Alisema mamlaka itaendelea kufanya awamu kadhaa za minada ya kielektroniki hadi hapo vitalu vyote vilivyopangwa kufanyiwa minada hiyo vitakapomalizika.

# TPDC yawaonya makandarasi wavivu mradi bomba mafuta

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SHIRIKA la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), limesema mkandarasi atakayebainika kutoa visingizio na kukwamisha ujenzi wa mradi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi mkoani Tanga ataondolewa.

Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dk.James Mataragio, alitoa onyo hilo jana baada ya kutembelea ujenzi wa kambi namba 11 inayojengwa Kijiji cha Ntondo, Mkalama mkoani Singida ambayo inajengwa na Nyanza Road Works Limited.

Kambi hiyo ambayo itakuwa na zaidi ya watu 500 ni kati ya kambi 14 zinazojengwa maeneo mbalimbali nchini na itatumika kuhifadhi mabomba yatakayokuwa yanachomelewa Sojo na baadaye yanatawanywa kwenye Mkuza. "Nitoe rai kwa makandarasi mhakikishe mnatimiza wajibu wenu na kama tukigundua mkandarasi ana visingizio ambavyo vitakwamisha kazi isiendelee tunamwondoa mara moja na tulishafanya hivyo Nzega," alisema.

Dk. Mataragio alisema mradi huo ni wa kimataifa, hivyo ni lazima makandarasi kufanya kazi kwa ufanisi na kumaliza ndani ya muda wa mkataba.

Alisema mradi huu ni mkubwa na kwamba utakuwa na manufaa makubwa kwa nchi, hivyo Watanzania hawana budi kuchangamkia fursa zitakazotokana na ujenzi wa bomba hilo ili kujiongezea kipato. Dk. Mataragio pia alitoa onyo kwa wananchi ambao watapata kazi kwenye mradi huu wajiepushe na tamaa zinazoweka kuukwamisha mradi kama vile wizi wa mafuta kwenye magari.

Alisema maeneo ambayo mradi unapita makandarasi wahakikishe wenyeji wanapewa kipaumbele kwa kupewa kazi ili na wao wanufaike. Kuhusu fidia, Dk. Mataragio alisema kazi ya kuwalipa wananchi ambao maeneo yao yamechukuliwa na mradi inaendelea na itakapofika Desemba, mwaka huu, ulipaji fidia utakuwa umekamilika kwa wananchi wote.

Alisema kwa mkoa wa Singida, zaidi ya wananchi ya 1,000 watalipwa fidia ya zaidi ya shilingi bilioni moja, huku wengine wakijengewa nyumba. Mmoja wa wanufaika kutoka Kijiji cha Ntondo, Juma Hamis, aliyejengewa nyumba ya kisasa aliishukuru serikali akisema kabla ya hapo alikuwa akiishi kwenye nyumba ya tembe. Hivyo, aliwataka wananchi wengine ambao mradi utawapitia wasisite kutoa maeneo hayo kwani faidi za mradi zitakuwa kubwa kwa nchi na kwa wananchi kwa ujumla.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (katikati), Mkuu wa Masuluhisho ya Mikopo kwa Afrika kutoka Benki ya Investec, Rowan King (wa pili kulia), Mkurugenzi wa Huduma za Mikopo ya Pamoja wa Benki ya Intesa Sanpaolo, Gustaaf Eerenstein (kushoto), Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Benki Kimataifa wa Bank One, Carl Chirwa (wa pili kushoto) na Meneja Mikopo Maalum Benki ya Biashara ya Mauritius, Hans Dallo, wakiweka mikono pamoja ikiwa ni ishara ya kuonyesha ushirikiano baada ya kutia saini jijini Dar es Salaam jana mikataba ya makubaliano inayoiwezesha Benki ya CRDB, kupata kiasi cha dola za kimarekani milioni 130 kwa ajili ya kukopesha sekta za biashara na wajasiriamali nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Siku ya Amani Duniani kufanyika Septemba 21

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU ya Amani Duniani inatarajia kuadhimisha Septemba 21, mwaka huu, ikiwa ni miaka mitatu tangu ilipopitishwa rasmi na Umoja wa Mataifa (UN) mwaka 2020.

Katika kuelekea siki hiyo, taasisi ya kimataifa isiyo ya kiserikali ya Heartfulness nayo inatarajia kufanya maadhimisho ya siku hiyo kwa kushirikisha takriban mataifa 113 duniani.

Mtaribu wa Heartfulness Tanzania, Gift Mwanga, anasema: "Maadhimisho ya Siku ya Amani Duniani yalianza mwaka 2020, kwa miaka miwili iliyopita yalijumuisha washiriki 53 duniani.

"Kwa mwaka jana hotuba zilizotolewa katika maadhimisho hayo yalitafsiriwa katika lugha zaidi ya 28 duniani, washiriki zaidi ya 30 walishiriki kupitia programu na matukio mbalimbali".

Alisema amani inahitajika katika maisha ya binadamu kila siku ikiendana sambamba na uwapo wa tumaini na mshikamano.

Mwanga alisema Siku ya Amani Duniani inamwezesha kila mtu kubadilika na kwamba kila mtu anapaswa kufurahi, hivyo Shirika la Heartfulness limeamua kutoka elimu ya uelewa kwa wananchi kuhusu amani.

Alisema kuelekea maadhimisho ya siku hiyo, kutakuwa na hafla mbalimbali zitakazofanyika ikiwamo michezo.

Pia alisema kuelekea maadhimisho hayo, mabalozi wa amani kutoka nchi mbalimbali watafanya programu mbalimbali kupitia mitandao na kwamba shughuli zote hizo zitaonekana kupitia www.peacefulness.org.

## Watakiwa kutumia mitandao kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imewataka wananchi wa Makambako mkoani Njombe kutumia huduma za mawasiliano kujiimarisha kiuchumi ndani na nje ya nchi.

Akizungumza katika gulio la wiki lililofanyika katika eneo la Soko Kuu la Makambako jana, Meneja wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wa TCRA, Mhandisi Asajile John, alisema mawasiliano yamerahisisha upatikanaji wa fursa mbalimbali zikiwamo za kiuchumi na kuleta faida kwa wale wanaotumia ipasavyo.

Mhandisi Asajile alisema katika ulimwengu wa sasa taarifa nyingi za uboreshaji wa huduma, biashara, masoko na kilimo zinapatikana mtandaoni, hivyo aliwataka wananchi wa Makambako kutumia fursa hizo kujiongezea kipato na kukuza uchumi wao na nchi kwa ujumla.

Alisema TCRA inaendelea na kampeni ya kuelimisha umma juu ya matumizi bora na salama ya huduma za mawasiliano ijulikanayo 'kwea kidijitali' inayoendeshwa nchi nzima.

Aliongeza kuwa wananchi wanapaswa kutumia simu kwa uangalifu kwani bila ya kufanya hivyo wanaweza kuingia katika makosa ya uhalifu kutokana na kutuma taarifa katika mitandao ya kijamii au kumpa mtu simu ambaye nia yake ni mbaya na kutumia kwenye matukio ya kihalifu.

Hata hivyo alisema kuwa wananchi wengi wanaotumia simu katika biashara zao wanafanya vizuri, kwamba hata Makambako kunafursa ya kufanya hivyo kutokana na biashara zilizomo ikiwamo ya mbao, kwa kujikita kutafuta wateja kwenye mtandao.

Mmoja wa wananchi wa Makambako, Ezekia Sanga alisema elimu waliyopewa na TCRA imefungua ukurasa mpya katika kutumia mawasiliano.

Alisema kuna baadhi ya masuala ambayo walikuwa hawafahamu lakini sasa wamepata mwanga mpya wa matumizi bora ya mawasiliano.

# Hakimu aruhusu mshtakiwa mauaji ya mama akapimwe

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imetoa ruhusa kwa mshtakiwa Innocent Peter (29), anayetuhumiwa kumuua mama yake mzazi kwa nyundo, kufanyiwa uchunguzi wa akili katika Hospitali ya Isanga, baada ya kuonekana ana shida kichwani.

Kabla ya kupanda kizimbani mshtakiwa huyo alionekana muda wote akizungumza mwenyewe bila kutoa sauti, huku akiwa anaandika kwenye makaratasi hadi muda wa kupanda kizimbani ulipofika alikuwa ameshajaza karatasi nyingi.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Jenifer Masue, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Joyce Minde, kuwa kesi ililetwa kwa ajili ya kusikilizwa na wapo tayari, lakini baada ya kuwasiliana na wakili wa mshtakiwa na kumwona Peter hali ya akili yake haiko sawa, aliomba Mahakama imruhusu Peter aende kufanyiwa uchunguzi katika Hospitali ya Isanga iliyopo mkoani Dodoma ili aweze kupitiwa matibabu na kesi iendelee.

Wakili wa mshtakiwa, Hashim Mziray, alikubaliana na ombi hilo kutokana na mteja wake kutoelewa chochote, ili haki ionekane inatendeka kwa pande zote mbili mshtakiwa akafanyiwe uchunguzi.

Hakimu Minde, aliuliza kama kuna ndugu yeyote wa mshtakiwa mahakamani na alisimama mtu anayedaiwa kuwa ni baba yake mzazi, aliyedai tatizo hilo lilianza akiwa na umri wa miaka 21 na kwa sasa ana miaka 29 yupo katika hali hiyo.

Akiendelea kujibu maswali ya hakimu, baba huyo ilidai alipoanza tatizo hilo walimpeleka polisi, wakaambiwa wampeleke Hospitali ya Mwananyamala, ambako walimshauri ampeleke Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Alidai daktari aliona Peter amejibu vizuri maswali yake na kuagiza achomwe sindano moja na kumuandikia dawa za siku 30 na kumrudisha nyumbani.

"Wakati nipo njiani kwenda kuchukua dawa hizo Muhimbili nilipigiwa simu kwamba nirudi nyumbani kwa sababu Peter amemuua mama yake," alidai.

Baada ya hakimu kusikiliza hayo, alitoa ruhusa ya Peter kwenda kufanyiwa uchunguzi katika Hospitali ya Isanga. Wakati yote yanaendelea mahakamani mshtakiwa alikuwa anaongea mwenyewe huku akishika shika vidole vyake.

Mshtakiwa anadaiwa Septemba 23, 2014 akiwa eneo la Kawe, Wilaya ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam, alimuua Ernesta Mboya.



Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, akifungua bomba kwenye moja ya vituo vya kuchotea maji Kijiji cha Mwamishoni, Kata ya Bubiki wilayani humo juzi, akiwa katika ziara yake ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maji. **PICHA: MARCO MADUHU**

# DC ampa siku 14 mkandarasi kukamilisha mradi

**Na Marco Maduhu, KISHAPU**

MKUU wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, amemwonya na kuipa siku 14 Kampuni ya Bent Company Ltd, inayojenga mradi wa maji wa Bupigi hadi Butungwa wilayani Kishapu kukamilisha kazi hiyo baada ya kuonyesha kusuasua.

Kutokana na mkandarasi huyo kuonyesha kujenga kwa kasi ndogo, Mkude alimtaka amalize kazi hiyo ndani ya wiki mbili.

Mkuu huyo wa wilaya juzi alifanya ziara ya kutembelea miradi ya maji wilayani hapo ili kuona utekelezaji wake na kuonyesha kutoridhishwa.

Alisema serikali inapotoa fedha za utekelezaji wa miradi ya maji lengo lake ni kuhakikisha wananchi wanaondokana na adha ya kutumia maji machafu.

"Mkandarasi ambaye unatekeleza mradi huu wa maji Bupigi hadi Butungwa hakikisha unaukamilisha ndani ya wiki mbili, wewe ni ndugu yangu tusiharibiane kazi," alisema Mkude.

"Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), hakikisha unausimamia vizuri miradi yote ya maji ili pesa zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan zitumike katika malengo yaliyokusudiwa ya kumtua ndoo kichwani mwanamke pamoja na kuondokana na adha ya matumizi ya maji machafu," aliongeza.

Pia alisema Wilaya ya Kishapu bado inakabiliwa na tatizo la upatikanaji wa majisafi na salama kwa wananchi kwa asilimia 60 na kwamba serikali itaendelea kutekeleza miradi hiyo ili wananchi wapate maji ndani ya mita 400.

Naye Meneja wa RUWASA Wilaya ya Kishapu, Dckson Kamazima, alisema mradi huo wa maji wa Bupigi hadi Butungwa unapaswa kukamilika Septemba 30, mwaka huu na kwamba atausimamia ili ukamilike kwa wakati.

Katika mradi huo ambao umegharimu Sh. milioni 499.5 utanufaisha wananchi 2,000 katika eneo hilo.

Aliwataka wananchi waitunze miundombinu ya maji ambayo inatekelezwa kwenye maeneo yao wilayani humo ili idumu kwa muda mrefu.

## Vishikwambi vya sensa kugawiwa kwa walimu

BUNGE limeelezwa kuwa serikali ina mpango wa kugawa vishikwambi vilivyotumika katika Sensa ya Watu na Makazi Agosti, mwaka huu, kwa walimu wote nchini.

Lengo la kugawa vishikwambi hivyo ni kuimarisha matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kwenye ufundishaji na ujifunzaji.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, alisema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Hawa Mwaifunga.

Katika swali lake, Mwaifunga alihoji nini mpango wa serikali kueneza matumizi ya TEHAMA katika kufundisha ili kuwaokoa walimu na matatizo ya mgongo na shingo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kipanga alisema ili kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji, kuanzia mwaka 2019/20 serikali kupitia Programu ya Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu (TESP) imeendelea kutoa mafunzo kwa wakufunzi wa vyuo vya ualimu kuhusu matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.


Aidha, alisema katika mwaka 2021/22 serikali kupitia Programu ya Mafunzo Endelevu kwa Walimu Kazini (MEWAKA) imewezesha mafunzo kwa walimu wa shule za msingi 30,400 yanayohusu matumizi ya TEHAMA kwenye ufundishaji na ujifunzaji.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alisema vishikwambi hivyo havitatosha nchi nzima kutokana na idadi ya walimu iliyopo na kuhoji serikali ina mpango gani wa kuongeza vifaa ili kuondokana na tatizo la shingo na mgongo kwa walimu na wanafunzi.

"Je, wanafunzi watakaofundishwa somo hili hasa kwa waliopo nchini," alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema vishkwambi vilivyotumika kwenye sensa ni 205,000 na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeongeza vingine zaidi ya 100,000 hivyo vitatosheleza kwa walimu wote.

"Serikali inaendelea na mchakato wa kuhakikisha kunakuwa na vifaa toshelezi na mwaka 2022/23 imeweka fungu kwa ajili hiyo," alisema.




Na Augusta Njoji, DODOMA

# Mwongozo jinsia jumuishi utumishi waja

OFISI ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, iko katika hatua za mwisho za kutoa mwongozo wa ujumuishwaji wa jinsia kwenye utumishi wa umma.

Aidha, Rais Samia Suluhu Hassan ameazimia kuhakikisha uwapo wa uwiano sawa wa kijinsia katika nafasi mbalimbali za uteuzi kipindi chake cha uongozi.

Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Deogratius Ndejembi, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Najma Murtaza Giga.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji sababu ya kukosekana uwiano wa jinsia ya kike kwenye nafasi za uteuzi na ajira nchini.

Akijibu swali hilo, Ndejembi alisema mwongozo huo unatoa maelekezo kwa mamlaka za ajira katika utumishi wa umma kote nchini kuhakikisha wanawake na wanaume wanakuwa na fursa sawa kuanzia katika mchakato wa ajira.

Pia alisema kwenye upandishaji madaraja, uteuzi, mafunzo, ubadilishanaji pamoja na urithishanaji madaraka.

"Lengo likiwa kuondoa vikwazo kwa kujenga uwezo wa ushindani kwa jinsi zote ili kupata sifa stahiki za kushika madaraka na fursa mbalimbali," alisema.

Awali, alisema serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha kunakuwapo na uwiano sawa wa kijinsia kwenye nafasi za uteuzi na ajira nchini kwa kuweka mazingatio ya usawa wa kijinsia katika nyaraka zinazosimamia utumishi wa umma.

Alitaja nyaraka hizo ni Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2008 inayotaka kila mamlaka ya ajira kuhakikisha uwiano wa kijinsia kwenye uteuzi na ajira zote, Sheria ya Utumishi wa Umma, 2019, Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009 na Kanuni za Uendeshaji wa Shughuli za Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma za mwaka 2021.



Baadhi ya mabalozi wa Umoja wa Ulaya (UE), wanaoziwakilisha nchi zao hapa nchini, wakiwa kwenye ukumbi wa Spika, wakifuatilia shughuli za Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Halmashauri zatakiwa kutenga fedha ujenzi nyumba za watumishi wa umma

SERIKALI imeagiza halmashauri zenye upungufu wa nyumba za watumishi kuendelea kutenga bajeti za mapato ya ndani kila mwaka ili kutatua tatizo la upungufu wa nyumba za watumishi.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Geita (CCM), Joseph Musukuma.


Katika swali lake, Msukuma alihoji lini serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi waliohamishiwa halmashaur mpya ya Nzera.

Akijibu swali hilo, Dk. Dugange alisema katika mwaka wa fedha 2021/22 serikali ilitenga Sh. milioni 150 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita na kwamba ujenzi wa nyumba hiyo unaendelea na uko katika hatua ya upauaji.

Sambamba na nyumba hiyo, alisema mwaka wa fedha 2022/23 Halmashauri ya Wilaya ya Geita imetengewa Sh. milioni 240 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba mbili za wakuu wa idara.

"Serikali inaielekeza Halmashauri ya Wilaya ya Geita na halmashauri zingine kote nchini zenye upungufu wa nyumba za watumishi, kuendelea kutenga bajeti za mapato ya ndani kila mwaka ili kutatua changamoto ya upungufu wa nyumba za watumishi," alisema.

Ukurasa 13




Chondechonde wawakilishi wetu kuna kesho!

BUFE
IJUMAA SEPTEMBA 16, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




**Yalivyo mapya neema ya diaspora kuwekeza mitaji eneo la nyumbani**

Ukurasa 12

MALIPO SASA HUKO HUKO WALIKO...

# Ofisi mpya TRA inayofuata kundi la wafanyabiashara waliosafiri Km. 130

- Katibu Tawala: Kilichokwepwa sasa kupatikana
- Kodi ya Sh. 150,000 'ilibambikwa' kuwa milioni

**Na Neema Hussein, KATAVI**

UNAPOTAJA Kata ya Majimoto, iko katika Halmashauri ya Mpimbwe Wilaya ya Mlele, mkoani Katavi. Ni sehemu ambako wafanyabiashara wa aina mbalimbali wakiwamo wa mazao kama vile mahindi, mpunga na mchele wanapatikana.

Pamoja na sura hiyo ya mzunguko mkubwa wa fedha, ni mahali ambako hapakuwa kabisa na huduma ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), hata kuonekana kupoteza mapato mengi ya kiserikali, hasa kutokana na kodi na ushuru kwa wafanyabiashara.

Wengi walishindwa kufika katika ofisi zilizoko makao makuu ya wilaya ya Mlele - Inyonga na makao makuu ya mkoa wa Katavi, Mpanda.

Hapo ndipo TRA ikaamua kuwasogezea huduma waliko, mfanyabiashara Jonas Amos akifafanua katika hafla ya ufunguzi: "Maana kabla ya hapo tulikuwa tukipata changamoto ya kusafiri zaidi ya kilomita 200 hadi 300 kwa siku, ili uweze kuipata hii huduma eneo la mkoani.

"Kuna wakati tulilazimika pia kwenda mkoani tulale hukohuko, hivyo ilituchukua gharama kubwa sana, lakini kwa sasa tumeokoa muda na tumeokoa fedha zetu, hatutahangaika tena."



Ofisi mpya za TRA Kata ya Mtemang'ombe, wilayani Mlele, Katavi katika siku ya ufunguzi.

Hapo Jonas anaieleza kuwa ni ishara ya mafanikio kwao wote, akiahidi uadilifu, vivyo hivyo akiwataka wafanyabiashara wenzake kuangukia mkondo huo, akinena zaidi: "Naelewa sisi wafanyabiashara kuna vitu vingi sana tulivyokuwa hatuvifahamu kuhusu TRA.

"Tunaomba sasa mtuelewe kutokana na uchanga wetu... mtupeleke taratibu, mwisho tutafika kule ambako mnataka tufike...kwa sababu ikifika sehemu tukianza kuiogopa TRA, kwa kweli haitapendeza inatakiwa TRA iwe rafiki kwetu."



Meneja wa TRA Mkoa wa Katavi, Jacob Mtemang'ombe. **PICHA ZOTE: NEEMA HUSSEIN**

Pia mfanyabiashara huyo ana changamoto ainenayo kwa mfano, kuwapo watu waliokuwa wanalipa kodi wastani kati ya Sh.150,000 hadi 200,000 huko nyuma, imeenda hadi shilingi milioni moja, hali iliyowafanya wakaandika barua kwa Meneja wa TRA wilayani na mkoa, wakamtaarifu mbunge wao, mkuu wa wilaya, ambaye akalazimika kuwafuata awasikilize.

"Hali hiyo ilituathiri sisi wafanyabiashara, kwa sababu watu walifunga biashara zao kwa kuogopa TRA," anasema Jonas na kuongeza hatua zilichukuliwa baada ya kikao cha pamoja, kodi ilikadiriwa upya na kurejeshwa viwango vya zamani.

"Lakini, kwa sababu mkuu wetu wa wilaya pamoja na mkoa kwa ujumla mlitoa tamko kuwa baada ya muda kutakuwa na ofisi ndogo (ya TRA) hapa kwetu Kata ya Majimoto, tunaipongeza serikali kwa wito huu.

"Kwa kweli, ukiangalia wataalamu wetu walikuwa wanachelewa kuja kukadiria mapato, badala ya kuja mwezi wa kwanza wanakuja mwezi wa nne, ambao tulikuwa tunajikuta tukiingizwa kwenye penati na kuleta mkanganyiko kwa wafanyabiashara na serikali yao," anafafanua Grace Udoba, ambaye ni mfanyabiashara, pia Diwani wa Viti Maalum.

**KUTOKA SERIKALINI**

Ofisa Biashara aliyemwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mpimbwe katika tukio hilo, Revocatus Mzumule, anasema ofisi hizo zinatoa fursa kubwa kwao halmashauri kuwaunganisha wafanyabiashara katika suala la utoaji kodi.

"Kabla ya uwepo wa hii ofisi hapa kulikuwa kuna changamoto kubwa sana, wafanyabiashara wengi walikuwa wakilazimika kwenda umbali mrefu sana kwa ajili ya kupata huduma ya TRA.

Pia uwepo wa hii ofisi kutafanya wafanyabiashara wengi wahamasike kwenye ulipaji kodi," anasema Mzumule.

Mgeni rasmi, Katibu Tawala wa Wilaya ya Mlele, Lincolin Tamba, anasema kufunguliwa kwa tawi la TRA kutarahisisha upatikanaji huduma ya walipa kodi, akiwataka wapatumie kadri inavyowezekana.

Jacob Mtemang'ombe ni Meneja wa TRA Mkoa wa Katavi, baada ya kuzindua ofisi hizo, amewataka wafanyabiashara hao waliokuwa wakisafiri zaidi ya kilomita 130 kufuata huduma za malipo ya kodi na wengine wakikwepa kulipa, sasa waanze upya maisha ya kulipa kodi katika mazingira rafiki.

Mtemang'ombe anasema, eneo hilo lina wafanyabiashara wengi na linakua kiuchumi, hivyo ni moja ya sababu ya serikali ikaamua kuwasogezea huduma hiyo karibu.

"Mpaka sasa tuna wafanyabiashara 550 ambao tumewasajili kwenye mfumo, lakini wako wengi zaidi ya hao, kwa sababu kama nilipoeleza hapo mwanzo, eneo hili halikuwa 'covered' (kuhudumiwa vilivyo) vizuri, kwa sababu ya umbali wa ofisi hii kuwa karibu, tunaamini tutawafikia walipa kodi walio wengi," anasema Mtemang'ombe.

UCHUMI

# Yalivyo mapya neema ya diaspora kuwekeza mitaji eneo la nyumbani

- Zama bado ziko jikoni zinafanyiwa kazi



Rais Jakaya Kikwete, alipokutana na Watanzania waIshio Marekani, katika mkutano jijini Dacota, Marekani mwaka 2011.



Rais Samia Suluhu Hassan.

**Na Nimi Mweta**

MAZINGIRA yanazidi kuboreshwa kwa uwekezaji unaoelekea kuwa raia wa Tanzania walioko nje au kwa upande mwingine, waliokuwa raia wa Tanzania ambao sasa ni wa nchi nyingine, wanachukua nafasi kubwa kuliko awali katika kukuza uchumi wa nchi.

Ni hali inayojidhihirisha kwa kuongezeka kasi ya kuingia fedha kutoka nje kwenda kwa watu binafsi, hali inayoashiria kuwa ni jamaa zao na zinapokuja kwa njia hiyo, ni fedha za kujikimu na kuiwainua katika mazingira yao yasifanane na illivyokuwa wakati raia hao wakiondoka nchini.

Siyo rahisi kusema kama hali hiyo ndiyo inayokusudiwa wakati serikali ikitoa miito ya kila mara katika mazungumzo na jamiii za Watanzania walioko nje, iwe ni katika ngazi ya ziara za mawaziri, au kama alivyokutana nao Rais Samia Suluhu Hassan huko Marekani, na watangulizi wake, akiwamo rais wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete.

Ni katika kipindi cha awamu ya nne, ambako mustakabali wa raia wa Tanzania nje ulijadiliwa kwa kina zaidi, ikiwemo kufanyika mkutano wa kimataifa jijini Arusha, uliohusisha viongozi muhimu wa jamii ya Wamarekani Weusi. Kimsingi, walitaka 'u-PanAfrica' utambuliwe, walioko nje wawe nchini na wengine wakitaka uraia wapate.

Haikuwa rahisi, kwani Tanzania haikufika hatua hiyo ya 'umajumui' kama baadhi ya wanaharakati wanavyopenda kutafsiri dhana ya Umoja wa Mwafrika, awe ndani ya bara au nje.

Uzalendo wa Tanzania ni wa kuangalia ndani ya nchi zaidi, kulinda mali na maslahi ya kiuchumi ya ndani, wakati walio nje, huenda baadhi zilizokuwa mali zao zilitaifishwa wakati wa Azimio la Arusha.

Wananchi wa ndani, baadhi wana ndugu na marafiki nje ya mipaka, ambao watataka wabinafsishiwe mali hizo, jambo ambalo imekuwa na taratibu ngumu namna ya kurahisisha miliki yake kwa taratibu za sura ya ndani na nje ya nchi.

Kwa majirani Kenya, ina sura rahisi zaidi kuifanya hilo la ubia wa ndani na ikubalike kirahisi. Kwao ni kawaida kuingia ubia kati ya serikali na kampuni za nje kujiendesha kibiashara kama wanahisa washirika, katika sura ya uzalendo wa kukuza uchumi na kumtambua mshirika kibiashara, mithili ya ndugu wa ndani na nje.

Katika mazingira ya sasa ya kutafuta uwekezaji kwa nguvu zote, ni wazi nafasi ya Diaspora itakuwa muhimu zaidi kuliko awali, ila upana unaowezekana na undani wa kuhusika kwao kiuchumi, bado iko katika sura ya mjadala.

Hapo ndiyo inatoa picha kwa kiasi fulani kuhusu kinachoendelea mawazoni mwao au katika hulka za kutumia fedha, ni kwa kiwango gani fedha zinaweza kuleta fedha, huku zina umuhimu gani sasa katika uchumi wa nchi?.

Takwimu za Wizara ya Mambo ya Nje zinaonyesha kuwa Watanzania walioko nje ya nchi, mwaka jana walituma Dola za Marekani 569.3 milioni (Sh. trilioni 1.327) nchini, ongezeko la asilimia 42 ikilinganishwa na kilichotumwa mwaka uliotangulia; ni ishara ya mabadiliko.

Inawezekana kuona ishara tofauti zinazojitokeza, kwamba kuna mwelekeo wa kutaka kuwekeza nyumbani bila kujali aina ya utawala au sera zilizopo, kwani yako maeneo ambayo kimsingi yanawezesha uwekezaji bila ya kujali undani wa sera, kwa mfano uraia wa nchi mbili.

Ni mradi wenye uwezekano wa muda mrefu, suala la uraia likawa siyo tatizo, hapo ikibeba maana kwamba hata Wachina waliomaliza mikataba ya kufanya kazi nchini muda mrefu uliopita, wanaamua kubaki

NAMNA UWEKEZAJI

Kinachoendelea, ananunua nyumba labda shilingi milioni 200 (miaka 10 iliyopita) anangonjea ardhi ipande thamani, apate mkopo na kujenga ghorofa, au anaingia ubia na mwenye nyumba.

Yako masuala ya utamaduni katika uwekezaji kutoka nje, ila kimsingi inakuwa rahisi zaidi pale walioko nje wanataka kurudi nchini, au kuna wageni kutoka nje ambao wanataka kubakia nchini.

Lakini msingi kuhusu uwekezaji ni hitaji la kukaa nchi fulani, kwani mtu anapotaka kukaa hupanga urithi wake kuwa hapo vilevile na hakuna urithi bora kama nyumba, kwani ni ardhi ambayo imethamanishwa, bila haja ya uwekezaji wa ziada.

Kuongezeka kupeleka fedha kwa jamaa zao walioko nchini, ni kielelezo kuwa wengi wanapata picha kuna mazingira mazuri ya kufanya biashara za kifamilia kuliko kipindi kilichotangulia, hivyo utumaji unakua kwa kasi zaidi.

Kuna eneo ambako siyo rahisi kusema ni uwekezaji wa kutumia jamaa walioko nje au ni uwakala, kwa maana kuwa watu wanaokaa nje au wenye jamaa walioko nje wanaingia uhusiano kibiashara kupanua shughuli za ubunifu au msambazaji wa aina fulani za bidhaa.

Si rahisi akawa mtu asiye na uhusiano wa kukaa kufungua biashara za aina hiyo, kwa mfano fremu za kuuza bidhaa zenye alama tambulishi, kuwa ni fasheni ya nchi hii au ile tena kwa ubunifu wa aina yake.

Kampuni ya kigeni inakuwa na haja ya msambazaji wa bidhaa zake, kuliko ikijaribu kuzimalizia nchini mwake. Hivyo, ni matawi ya usambazaji bidhaa kama yalivyo ya kuuza magari au spea zake.

Uwepo wa raia wa Tanzania ughaibinu wanaoweza kuwa na uraia, mathalan Marekani au kwingineko wakasaidia upenyo wa 'diplomasia ya uchumi' kwa uwekezaji, licha ya kuwa ngumu kwa wakazi kama hao kuanzisha uwekezaji mkubwa.

Uwekezaji wa aina hiyo, unatokana na kampuni kubwa kuhitaji kupanua shughuli zake, kwa mfano kujenga kiwanda cha kuunda magari nchini, ambako inaweza kutafuta ubia na kampuni kubwa za ndani.

Mfano ni zile zenye ardhi kwa ajili ya biashara kama hiyo na ziweze kupata mkopo wa uendeshaji, kama sehemu ya mchango wake katika mtaji.

Pale ambako siyo rahisi kupata mkazi mwenye asili ya Tanzania katika nchi fulani, wawakilishi wa nchi kama hiyo wataangalia kati ya wafanyabiashara waliopo, yule mwenye uelekeo wa kitamaduni, unaoendana na nchi hiyo awe kama mwakilishi.

Ndivyo inavyoangukia historia kama Mtanzania kama Balozi Ami Mpungwe alivyostaafu kazi serikalini mapema zaidi na kuwa mwakilishi wa kampuni za Afrika Kusini katika maeneo tofauti, hasa viwanda na madini.


Iran pia imegundua mshirika ambaye kampuni yake kubwa ina nembo ya nchi hiyo, Caspian, bahari iliyoko mashariki ya nchi hiyo na Iran haina ushindani wa kitamaduni kutoka nchi nyingine za ufukwe wa bahari hiyo; hazina upenyo kibiashara.




Watanzania waishio jijini Brussels, Ubelgiji, wakimlaki Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Chondechonde wawakilishi wetu kuna kesho!






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

KUNA hadithi au simulizi inasema mtu akifariki dunia huenda mbinguni. Afikapo huko, si kwamba amefika na yamekwisha la hasha. Inasema atapimwa na Malaika wa Mungu kama duniani alikuwa mcha Mungu au vinginevyo.

Akibainika alikuwa mcha Mungu, basi hukaribishwa peponi, kinyume chake hurejeshwa duniani akiwa katika umbo na sura ya mnyama. Simulizi hii ambayo naambiwa imo kwenye vitabu vitakatifu, inafikirisha.

Inafikirisha, kwa sababu inamfanya binadamu ajiandae kwa moja kati ya haya mawili, ama kupata makazi ya kudumu milele peponi, au arejeshwe duniani akiwa katika umbo na sura ya 'kitimoto' au nguruwe mwitu.

Na ujue ukirudishwa duniani kwa sura ya mnyama huyo, ujiandae kuwa kitoweo au kisusio cha binadamu, ambao watakuwa wanaendelea na maisha yao duniani wakiwamo wa mwagiliaji moyo, ambako utakuwa nyama choma.

Hivyo, kwa kuzingatia simulizi hiyo, ina maana wanyama tuwaonao duniani walipata kuwa binadamu huko nyuma, ingawa pia inaacha maswali ya kujiuliza kama mtu akifariki duniani na kuzikwa huenda wapi, kwani akifukuliwa baada ya muda hukutwa mifupa. Ushahidi ni pale Olduvai Gorge.

Lakini, utakapotaka kuhoji kwanini mifupa iko pale wakati tulishaambiwa tunakwenda mbinguni, jibu rahisi ni kwamba kiendacho mbinguni ni roho.

Hivyo, roho ya mcha Mungu ndiyo hubaki peponi na ile ya mchana Mungu ndiye roho yake hurejeshwa kwenye mwili wa 'kitimoto' au nguruwe mwitu.

Nachofikiria hapa ni kwamba, hivi kutokana na amri tuliyopewa binadamu wakati Mungu anaumba dunia na mbingu akasema enendeni duniani na mkavitawale vyote vilivyomo, ikawa ndiyo idhini ya kuchinja na kula wanyama wasioweza kujitetea, siku wakiamua vinginevyo tutaishi wapi?

Fikiria siku wanyama na ndege watakapopewa uwezo wa kuzungumza na kulumbana nasi, wakisema kwamba sasa utawala wa binadamu kwa wanyama basi, tutakuwa wapi? Siku wakiamua kwamba hatuchinjwi wala kuchunwa au kunyonyolewa na kukatwa katwa itakuwaje?

Kwamba wanyama chini ya viongozi wao wakaitisha mkutano mkubwa na kutangaza kuwa kuanzia sasa tumechoka ngozi zetu kutumiwa kutengeneza mabegi, viatu, mikanda na ngoma, kwamba pembe zetu sasa zisitengenezwe vishikizo vya nguo na mifupa yetu iachwe isitengenezwe vikombe itakuwaje?

Eti kwamba kuanzia sasa kinyesi chetu kiache kuitwa mbolea ya kumwagwa mashambani na binadamu kulima mahindi, kuvuna na kuyasagisha na kuja na unga wa kusongea ugali ambao hatimaye utaliwa na nyama zetu!

Ndege na wanyama watasema kuanzia leo hatutaki manyoya yetu yatengenezee mavazi. Bila shaka utakuwa ni ukombozi wa wanyama hao, dhidi ya kunyanyasika kwa binadamu.

Hivyo, kama simulizi hizi zinaaminika, ina maana mimi na wewe ipo siku hatutakuwa duniani kama binadamu, bali kama wanyama, si ajabu wewe ukarudishwa nyumbani ukiwa ng'ombe, mimi mbwa na yule na mwingine kama fisi au mbweha.

Yote hayo yatategemea ulikwenda mbinguni ukiwa na tabia gani na ndivyo ukirejeshwa duniani tabia yako ndiyo itarejeshwa kwa mnyama ambaye anastahili kuwa ulivyokuwa. Pengine inawezekana fisi ni binadamu wa zamani waliokuwa walafi.

Yawezekana nguruwe ni binadamu wa amani aliyekuwa na sura mbaya na hata faru na kiboko, huku tembo akiwa ni binadamu aliyekuwa mbabe mtaani na kadhalika. Hivyo, tabia yako ya sasa ndiyo inaakisi utakuwaje miaka hiyo ya kurudi duniani.

Sasa basi, kama tutaamini hivyo, tujue kuwa tunapokuwa hapa duniani tujitahidi kutenda mema na kuwatendea mema wenzetu. Hivyo basi, ninyi wawakilishi wetu katika vyombo mbalimbali vya kiutawala, jaribuni kuwafikiria watu wenu kwa mnayoyafanya.

Mkikumbuka kuwa kuna kurudi duniani baada ya kufariki dunia, haya mnayoyafanya fanyeni mkimpendezesha Mungu, pia watu wenu ambao ni viumbe wa Mungu hapa duniani. Wabunge wetu ni miongoni mwa wawakilishi wetu, hivyo tufikirieni jamani.

Mnapokuwa 'mjengoni' na kujadili mambo, jadilini mkivaa viatu vyetu sisi wanyonge huku nje ambako ndiko duniani kwetu, kumbukeni mtatoka huko mrudi huku muishi nasi.

Hivyo, mnayoyaamua yaamueni mkijua mtakuja kuyaishi siku moja. Msiamue kwa kututoa machozi sisi, haya mambo ya tozo na mengine, ni miongoni mwa mnayotuumiza nayo. Fikirieni kabla ya kuamua. Alamsiki!

FEDHA

## MIAKA SITA MAMLAKA YA WANYAMAPORI

# Kamishna wake afunguka 'wanavyoupiga mwingi' baada ya kuhamia elektroniki porini

- Vitalu kwa soko, mapato sasa kufuru
- Yakabidhiwa kulea malikale za kitaifa



Wanyama wakiwa katika mandhari ya porini, ambako wako chini ya uangalizi wa TAWA.
**PICHA ZOTE: MAKTABA**

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), mwaka huu inatimiza miaka sita tangu kuanzishwa, ikiwa tayari na nuru ya mafanikio katika safari yake ya kusimamia wanyamapori.

Ikiwa imeanzishwa kwa kivuli cha Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori ya Mwaka 2009 na marekebisho yaliyofanywa miaka sita baadaye, chombo hicho kilianza kazi rasmi Julai Mosi ya mwaka 2016, ikiwa msimamizi mkuu wa rasilimali za wanyamapori nje ya Hifadhi za Taifa na Hifadhi ya Ngorongoro.

Ni katika miaka sita hiyo, tayari ina sifa lukuki za mafanikio, lakini kikuu kinaendana na dunia ya kidigitali inayoshika kasi hivi sasa na hasa katika usiamamzi wa wanyamapori kielektroniki.

### KAMISHNA UHIFADHI

Kaimu Kamishna wa Uhifadhi wa TAWA, Mabula Nyanda, anasema ugawaji vitalu, uwindaji wa kitalii unafanyika kielektroniki, ukiwa na mafanikio mengi na umeiingizia serikali mapato makubwa.

Anautakia kuwa ni utaratibu ulioanzishwa mwaka 2019 ukiwa na viashiria vingi vya tija kwenye biashara hiyo, akiufananisha na unaotumika katika mataifa mengine duniani, akitaja mfano wa Afrika; Zimbabwe, Zambia na Namibia.

"Njia hii ya kugawa vitalu vya uwindaji wa kitalii inatoa fursa kwa kampuni za uwindaji wa kitalii kutoka ndani na nje ya nchi," anasema.

Pia anafafanua kwamba, malengo yaliyoko sawa katika mpango mkuu wa kiserikali ni kupatikana idadi ya watalii hadi milioni tano ifikapo mwaka 2025.

Anasema ugawaji vitalu vya uwindaji kwa njia ya mnada umesaidia kutoa fursa sawa ya ushindani kwa kampuni zote zenye sifa kupatiwa kitalu cha kuwindaji, kwa njia ya mnada, ikilinganishwa na utaratibu uliotumika awali.

Mabula anasema, ni utaratibu unaoongeza uwazi na uwajibikaji katika ugawaji wa vitalu vya uwindaji wa kitalii, kuleta ufanisi katika tasnia hiyo, pia kuwezesha ugawaji vitalu vilivyorejeshwa vinavyoonekana kutofaa kwa uwindaji wa kitalii.

Mabula anasema utaratibu huo umeshaleta faida ya ongezeko la ada ya vitalu kwa wastani wa asilimia 174, akitumia tarakimu kwamba, awali ada ya kitalu cha daraja la kwanza ilikuwa Dola za Marekani 60,000 (Sh.milioni 141), sasa imeongezeka na kuuzwa kati ya Dola za Marekani 151,000 (Sh. milioni 354.85) hadi 285,000 (Sh. milioni 669.75).

Aidha, Mabula anasema ada ya kitalu cha Daraja la Pili imeongezeka kutoka Dola za Marekani 30,000 (Sh. Sh. milioni 70.5) na kuuzwa kati ya Dola za Marekani 81,000 (Sh. milioni 190.3)- hadi 250,000 (Sh. Sh. milioni 587.5 ); kitalu cha daraja la III kutoka dola za Marekani 18,000 (Sh.milioni 42.3) na kuuzwa kati ya Dola za Marekani 31,000 (Sh. milioni 72.85) hadi 255,000. (Sh. milioni 599).

Anautaja ni utaratibu unaosababisha kuongezeka ushindani katika soko la vitalu vya uwindaji kitalii, kwa kuzingatia ubora na daraja la kitalu.

Mabula anasema, Mamlaka ya Wanyamapori iliandaa mwongozo wa ugawaji vitalu vya uwindaji wa kitalii kwa njia ya mnada, pamoja na mfumo wa kielektroniki kufanikisha ugawaji vitalu hivyo.

"Tangu kuanza kwa ugawaji wa vitalu kwa njia ya mnada mwaka 2019, TAWA imeshaendesha jumla ya minada saba ya vitalu vya uwindaji iliyohusisha vitalu 100 hadi kufikia Machi, 2022 na katika awamu zote saba ambazo mnada ulifanyika, jumla ya vitalu 79 kati ya 100 viliuzwa kwa kiasi cha Dola za Marekani 9,798,000 sawa na Sh. bilioni 23," anafafanua.

Anaeleza mapato hayo ni makubwa maradufu, kuliko kilichopatikana awali kwa uuzaji vitalu vyote 79 kwa njia ya awai ya kiutawala, ambayo wangeambulia Dola za Marekani 3,306,000. Sasa kuna ongezeko la asilimia 196.4.

Mabula anaahidi kwamba, Mamlaka ya Wanyamapori, itaendelea kufanya kwa awamu kadhaa za minada ya kielektroniki hadi hapo vitalu vyote, vilivyopangwa kufanywa minada hiyo vitakapomalizika.

### MAJUKUMU MAHSUSI

Anataja majukumu ya msingi ya TAWA, ni kuhifadhi, kusimamia na kuendeleza rasilimali ya wanyamapori nje ya Hifadhi za Taifa na Eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, kwa kusimamia Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu na kusimamia sheria, ikizuia ujangili wa wanyamapori.

Mabula anasema, pia kuna jukumu la ulinzi na usimamizi shoroba za wanyamapori, maeneo ya mtawanyiko ardhi oevu, maeneo ya wazi yenye wanyamapori kwa kushirikiana na wadau na taasisi nyingine za uhifadhi.

Anataja mengine ni uangalizi na usimamizi wa wanyamapori katika ardhi za vijiji, Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori-WMAs, bustani za wanyamapori (Zoos), mashamba na ranchi za wanyamapori.

Mabula anaeleza kazi ya kutatua migogoro baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu, kwa kushirikiana na wadau na taasisi nyinginezo za uhifadhi, wakishirikisha wegine wote wanaoguswa katika masuala yanayohusu uhifadhi wa wanyamapori.

### KUKARIBISHA UWEKEZAJI

Anataja lingine liko katika kushirikiana na sekta binafsi na wananchi, kuainisha fursa za uwekezaji zitokanazo na rasilimali ya wanyamapori, kutoa, kuhuisha na kusitisha au kufuta vibali na leseni za matumizi ya wanyamapori;

Pia Mabula anataja wajibu wa wao kuelimisha wadau umuhimu wa wanyamapori, pia kwa ushirikishaji katika uhifadhi na kuwanufaisha raslimali ya wanyamapori. Hapo wanashiriki kutekeleza mikataba ya kikanda na kitaifa na kuzingatia utawala bora katika usimamizi wa wanyamapori.

### MSIMAMIZI WA MALIKALE

Mabula anaeleza wajibu mwingine wanaoubeba, ni kujenga na kuimarisha uwezo wa mamlaka hiyo, katika kusimamia wanyamapori na kwamba kupitia Tangazo la Serikali la Agosti 14, mwaka 2020, TAWA imekasimiwa jukumu la kusimamia maeneo ya Malikale ya Kilwa Kisiwani, Songomnara, Sanje ya Kati na Majoma na Kunduchi.

"Mamlaka ilipokea jukumu hilo na kuanza kuendeleza maeneo hayo kwa kuboresha miundombinu pamoja na kuwezesha usimamizi wa shughuli za kila siku.

"TAWA inasimamia maeneo yenye ukubwa wa jumla ya kilomita za mraba 136,287.06 yanayojumuisha Mapori ya Akiba 27 yenye ukubwa wa kilomita za mraba 97,187.06 na mapori tengefu 25 yenye ukubwa wa kilomita za mraba 39,100," anasema.

Aidha, anasema TAWA ni mwangalizi wa shughuli za usimamizi wa wanyamapori kwenye maeneo 21 ya Jumuiya tatu za Hifadhi za Wanyamapori (WMA) zenye ukubwa wa jumla ya kilometa za mraba 28,223.13.

Anafafanua kuwa TAWA inasimamia ufugaji wa wanyamapori katika mashamba sita; bustani za wanyamapori 29; ranchi tano; na maeneo matano ya kuzalisha wanyama na viumbe.

Mabula anaeleza kuwa, tangu kuanzishwa kwake, imeendelea kutekeleza majukumu yake ikizingatia malengo makuu matatu kama yalivyoainishwa katika mpango mkakati wake wa miaka mitano; 2018/19 hadi -2022/23.



Askari wa wanyamapori wakiwa kazini.



# Waomba fidia eneo kutwaliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

ZAIDI ya wakazi 500 wa Mtaa wa Kitekela jijini Dodoma, wameiomba serikali kuwalipa fidia baada ya eneo walilokuwa wanaishi na kulima lenye ukubwa wa hekta 1,002 kutwaliwa na serikali.

Wakizungumza juzi kwenye mkutano wa hadhara, baadhi ya wananchi walisema tathmini ya fidia ilishafanyika hivyo wakatakiwa kutoendeleza shughuli za kijamii kama mazishi, ufugaji na kilimo.

Yohana Pius, mmoja wa wakazi hao, alisema baada ya kuzuiwa kufanya shughuli za maendeleo, wamekaribisha njaa ilihali ardhi yenye rutuba ikiwa imechukuliwa na watu wengine bila kuelezwa sababu za msingi.

Alisema walizuiwa kufanya hivyo tangu mwaka 2021 lakini kwa sasa hakuna kinachoendelea na muda wa ulipaji fidia kisheria umepita.

"Walipotupa zuio mwaka jana walisema wangelipa ndani ya miezi sita lakini hadi sasa hakuna kinachoendelea zaidi sisi kufa njaa kwa sababu hatulimi mashamba yetu tuliyoyategemea," alisema Yohana.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Mtaa huo, Samwel Robert, alisema Aprili 30 mwaka 2021 uongozi wa Chuo cha Usafirishaji walifika Serikali ya Mtaa huo kutaka kutwaa eneo lenye makazi ya watu, majengo, sehemu za makaburi na mashamba kwa ajili ya ujenzi wa chuo.

Robert alisema suala hilo walikubali baada ya kuwashirikisha wananchi wake na walikubaliana kuwapa eneo la wazi na kwamba ekari moja ingelipwa fidia ya Sh. milioni sita.

"Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji ilitoa barua ikiwatambulisha kuhusu uthamini wa fidia ya wananchi na muda mfupi walifanyiwa uthamini huu ambao walipewa ushirikiano wakiahidi kulipa ndani ya miezi sita.

"Baada ya kukaa na sintofahamu hii kwa muda mrefu na kufuatilia bila mafanikio, ni wazi sasa kwamba viongozi wa ngazi ya juu wanatakiwa kuja kutoa majibu ya nini kifanyike ili kuondoa sintofahamu hiyo," alisema.

Naye Katibu wa Kamati ya Ufuatiliaji, Mussa Daniel, alisema wamefanya jitihada mbalimbali za kufuatilia lakini hadi sasa hazijazaa matunda na kuomba Rais Samia Suluhu Hassan kusaidia suala hilo.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, alisema ardhi inatwaliwa kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizowekwa, hivyo wananchi ambao hawajalipwa fidia zao na muda ukiwa umekwenda, sheria inachukua nafasi yake.

Shekimweri alisema katika maeneo yote ambayo uthamini umefanyika lakini muda wa miezi sita kisheria umepita, wanaruhusiwa watu kuendelea na shughuli zao na kwamba wahusika wakiwa tayari kwa sababu muda umepita inabidi kufanya tathmini upya.

"Kama hayo hayajafanyika bado wana umiliki halali hivyo wala wasiingie wasiwasi inamtaka mhitaji kulipa fidia ndani ya miezi sita baada ya kusainiwa kwa jedwali la fidia na kufanyiwa tathmini na mthamini Mkuu wa Serikali," alisema Shekimweri.

Hata hivyo, alisema ofisi yake haijapokea jedwali la ulipaji wa mantiki hiyo anaamini kuwa ardhi ile bado ni mali ya wananchi na kumtaka mwekezaji kama ana dhamira ya kuchukua ardhi hiyo kufanya haraka ili wananchi wasiendelee kuathirika.

Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) Prof. Zakaria Mganilwa, alisema tathmini ilishafanywa na jambo hilo liko Hazina kwa ajili ya ukamilishaji wa taratibu za malipo.

# Wasichana, vijana wapewa bil. 1.8/- mradi kujengewa uwezo kujiamini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetoa zaidi ya Sh. bilioni 1.8 kwa wasichana balehe na wanawake vijana 3,287 wa mkoa wa Dodoma, kwa ajili ya kuandaa miradi ya kuwajengea uwezo wa kujiamini na kujiimarisha kiuchumi ili kujiepusha na maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU).

Mratibu wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS) Mkoa wa Dodoma, Eriko Kawanga, aliyasema hayo jana kwenye ziara ya kamisheni ya Ukimwi katika Wilaya ya Kondoa mkoani hapo walipokuwa wakikagua utekelezaji wa mradi wa Timiza Malengo unaotekelezwa na TACAIDS.

Alisema mbali na wasichana hao pia mafunzo ya elimisha rika yalitolewa kwa vijana 628.

Kuhusu maambukizi ya VVU kwa mkoa wa Dodoma, mratibu huyo alisema watu 52,842 wamehisiwa kuishi na maambukizi hayo huku Halmashauri ya Jiji la Dodoma na Wilaya ya Kongwa zikionyesha kuwa na idadi kubwa ya maambukizi.

"Huduma za jipime zimeonekana kuwa na changamoto sana kwa watu kutokana na ni jambo geni lakini sasa tunahamasisha watu wajipime badala ya kurundikana kwenye vituo vya afya waweze kujipima wenyewe," alisema.

Alisema vitendanishi 4,379 vilisambazwa kwenye jamii na kuonekana vilirudi 2,114 ambapo watu 15 walibainika kuishi na VVU. Kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, alisema kati ya vituo 356 vinafanya kazi na wajawazito 130,200 walipimwa VVU na 1,035 walikutwa na maambukizi.

Naye Mwenyekiti wa Kamisheni, Dk. Hedriga Swai, alisema mradi huo umesaidia watoto wa shule za msingi na sekondari na wale walio nje ya shule ambao wanatoka katika mazingira magumu kuweza kujitambua.

"Kwenye shule zimeanzishwa klabu sisi kama kamisheni tumefurahishwa na utendaji kazi wa TACAIDS, tumetembelea mabaraza ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na VVU (Konga) ambayo ina miradi mingi lakini imefanikiwa kuwarudisha wenzao 104 waliacha dawa za kufubaza virusi vya Ukimwi," alisema.

Alitoa wito kwa watu wanaoishi na VVU kujiunga kwenye konga na kuchangamkia miradi ya timiza malengo kwa kuwa inasaidia kujikwamua kiuchumi hasa kwa wanawake.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema kuna kazi kubwa ya kuelimisha vijana wa mkoa huo kwa kuwa takwimu za mimba za utotoni kuonyesha ni mkoa wa sita.

"Kama watoto wanapata ujauzito kwa maana hiyo hawachukui hata tahadhari, ukichanganya kuja kwenye VVU ni changamoto pia inatakiwa tushikamane kuiondoa," alisema.

Hata hivyo, alisema elimu ya watu kujipima VVU kwa Dodoma ipo chini kutokana na watu kuwa na uoga.

"Inahitaji watu kuwa na elimu ya kujitambua kujipima wenyewe, watu wajiamini," alisema.

Mmoja wa wanufaika wilayani Kondoa, Hawa Salum, alisema mwaka 2018 alipata ujuzi mbalimbali kupitia mradi huo na alipopatiwa fedha alifanikiwa kuongeza vitendea kazi.

Alisema kwa sasa anamiliki saluni na kusaidia kukidhi mahitaji ya familia yake na kumlea mtoto wake.



Wauza mitumba wa eneo la Nyerere Square katika Jiji la Dodoma, wakiwa wamekusanyika jana, wakisubiri kupatiwa vitambulisho kutoka kwa viongozi wao, vitakavyowawezesha kufanya biashara kwenye soko jipya la wazi la Machinga Complex, lililoko Barabara ya Bahi, jijini humo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Madiwani Zanzibar wafanya ziara mafunzo kuhusu utekelezaji miradi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MADIWANI wa Manispaa ya Mjini Unguja wamefanya ziara ya kujifunza utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa soko la wazi la machinga lililojengwa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Akizungumza kwa niaba ya madiwani 16 kutoka manispaa hiyo jijini hapo, Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria ambaye ni Diwani wa Kikwajuni, Ibrahimu Hamisi Fataki, alisema ziara hiyo imewasaidia kujifunza uendeshaji wa miradi mbalimbali ambayo mapato yake ya ndani yamekuwa yakitumika kwa nidhamu ya fedha.

"Tulichojifunza kwenye ziara hii kwa wenzetu makusanyo yao kwa kupitia miradi yao wanatumia kwa nidhamu hali ambayo inaonekana kuwapo kwa maendeleo makubwa na yenye viwango vya hali ya juu," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Mipango Miji, Kinuru Rashidi Salumu, alisema wataenda kubadilisha utekelezaji wa ukusanyaji wa mapato ili kufikia mabadiliko hayo.

Naye Mchumi wa Jiji la Dodoma, Amani Ng'oma, alisema madiwani hao walitembelea kitega uchumi cha hoteli iliyoko Mji wa Kiserikali Mtumba, soko la wazi la Machinga na Hoteli ya Dodoma.

Alisema madiwani hao wameona namna ya Jiji la Dodoma linavyotekeleza miradi yake na kufanikisha kutumia mapato yake ya ndani kwa umakini mkubwa.

Alifafanua Halmashauri ya Jiji imekuwa ikitumia mapato yake ya ndani kwa asilimia 70 kwa utekelezaji wa miradi na asilimia 30 ya matumizi ya kawaida.



# Mbeya yatimiza malengo Sensa ya Watu na Makazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MRATIBU wa Sensa ya Watu na Makazi mkoani Mbeya, John Lyakurwa, amesema mchakato huo mkoani Mbeya umefanikiwa kwa asilimia 100 ikilinganishwa na malengo ambayo yaliwekwa awali.

Aliyasema hayo juzi wakati wa kikao cha tathmini ya Sensa ya Watu na Makazi katika mkoa huo, akieleza kwamba mchakato huo umefanikiwa kwa kiwango kikubwa kutokana na ushirikiano wa wadau mbalimbali.

Lyakurwa alisema awali walitegemea kuzifikia kaya zaidi 500,000 lakini walizifikia kaya 600,000 na katika mkoa huo hakukuwa na matatizo makubwa ambayo yangekwamisha mchakato huo.

"Tatizo lililotokea ni kwenye sensa ya makazi ambapo tulijiwekea makadirio makubwa kuliko uhalisia hali ambayo imetufanya tufikie asilimia 92," alisema Lyakurwa.

Alisema moja kati ya matatizo madogo ambayo yalitokea kwenye utekelezaji wa mchakato huo ni baadhi ya makarani kupata matatizo wakiwa kazini.

Baadhi ya viongozi waliohudhuria kikao hicho walisema taarifa ya sensa hiyo zitakapotoka zitasaidia kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ndani ya maeneo hayo.



Balozi wa Marekani nchini, Donald Wright (wa pili kushoto) na Mwenyekiti wa Bodi ya The Pula Group, Balozi Charles R. Stith (wa pili kulia), wakikata utepe kuzindua ofisi mpya ya The Pula Group, katika jengo la G.M and Company Kawe, mkoani Dar es Salaam jana. Kushoto ni Rais wa The Pula Group, Dk. Mary Stith na Mkurugenzi Mtendaji wa G.M & Co, Gabriel Kassai. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TARURA yaingia mikataba 92 ujenzi barabara h'shauri

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKALA wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) Mkoa wa Mbeya, umetiliana saini mikataba 92 na makandarasi kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwenye halmashauri za mkoa huo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Akizungumza wakati wa kuingia kwa mikataba hiyo, Meneja TARURA MKoa wa Mbeya, Wilson Charles alisema mikataba hiyo ina thamani ya Sh. bilioni 20.5 ambazo zinatokana na vyanzo mbalimbali vya fedha.

Alivitaja vyanzo vya mapato kuwa ni mfuko wa barabara, mfuko wa jimbo, tozo za petroli na diseli na maombi kutoka maeneo mbalimbali.

Charles alisema mikataba hiyo ni sehemu ya mikataba yote kwa maelezo kuwa mingine ilishuhudiwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Miradi yote hii itatekelezwa kwenye halmashauri zote za mkoa wetu, tutahakikisha miradi hii inatekelezwa kwa viwango vinavyostahili, miradi hii inalenga kuboresha miundombinu ya barabara ndani ya mkoa wetu," alisema Charles.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwataka makandarasi waliosaini mikataba hiyo kuhakikisha wanafanya kazi kwa kuzingatia muda wa miradi hiyo ili kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria endapo watashindwa kukamilisha miradi.

Alisema muda utakapokuwa umekwisha hakutakuwa na nyongeza, hivyo ili kuepuka kuanza kuomba kuongezewa muda ni lazima wafanye kazi usiku na mchana.

Homera aliwataka makandarasi hao kutekeleza miradi hiyo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa ili thamani halisi ya fedha zilizotengwa ionekane.

Aliwataka makandarasi hao kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi ni lazima wakaripoti kwa viongozi wa maeneo ya miradi ili kupata ushirikiano ambao utasaidia miradi kukamilika vizuri.

"Mkafanye kazi kwa uaminifu kwenye miradi hii na hakikisheni mnatekeleza miradi hii kwa kuzingatia ubora na muda uliopangwa, halitakuwa jambo jema kuanza kuchukuliana hatua za kisheria baada ya muda kuisha," alisema Homera.

Baadhi ya makandarasi waliosaini mikataba hiyo waliishukuru serikali kwa kuwaamini kufanya kazi hizo na wakaahidi kuwa watatekeleza kwa viwango vinavyostahili.

Mmoja wa makandarasi hao, Esther Msiu alisema awali serikali ilikuwa inawaamini zaidi makandarasi wa kigeni lakini kwa sasa imeanza kuwaamini hata wazawa.

Alisema ili kuishawishi serikali kuendelea kuwaamini watahakikisha wanafanya kazi kwa kuzingatia taratibu na miongozo ya utekelezaji ili kuhakikisha inakuwa na viwango.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Lodrick Mpogolo aliwataka makandarasi hao kuwa waaminifu na kuhakikisha wanashirikiana na vizuri na wananchi pamoja na serikali za mitaa za maeneo watakayokuwa wanatekeleza miradi.

Alisema serikali itakuwa inafuatilia kwa karibu miradi hiyo ili kuhakikisha inatekelezwa kwa viwango vinavyostahili.

# Agizo la Makamu wa Rais laanza kufanyiwa kazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UTEKELEZAJI wa maagizo ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango kwa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) wa kukamilisha ujenzi wa kituo cha kusubirisha magari na barabara ya mchepuko kwenye mteremko wa Inyala nje kidogo ya Jiji la Mbeya mbioni kukamilika.

Dk. Mpango alitoa agizo Septemba 11, mwaka huu, alipotembelea eneo hilo ambalo lina mteremko mkali.

Pia eneo hilo limekuwa na matukio ya mara kwa mara ya ajali ambazo zimekuwa zikigharimu maisha ya watu, kwamba alitaka maeneo hayo yatumike kama njia za awali za kupunguza ajali.

Pia aliagiza malori na magari madogo yaendelee kupita kwenye mteremko huo kwa awamu ili kupunguza madhara ya ajali ambazo zimekuwa zikitokana na malori kufeli breki kwenye mteremko huo.

Jana Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya ilitembelea eneo hilo ikiwa ni siku moja baada ya kutokea kwa ajali iliyosababisha vifo ya watu watatu akiwamo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Igunga mkoani Tabora, Fatma Omary Lattu.

Kamati hiyo ilizindua barabara ya mchepuo ambayo kwa mujibu wa TANROADS Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Matali Masige imekamilika kwa asilimia 100 na iko tayari kuanza kutumika kwa magari ya aina yoyote, huku vituo vya kusubirishia magari vikiwa vimefikia asilimia 50.

Masige alisema barabara hiyo imekamilika na kuzinduliwa ikiwa ni siku nne pekee tangu Makamu wa Rais alipotoa maagizo ya kukamilisha ndani ya siku 10.

Alisema kwa sasa wanaendelea na ujenzi wa vituo viwili vya kusubirishia magari kwenye mteremko huo kwa kiwango cha lami na kwamba vituo hivyo vyote vina urefu wa zaidi ya mita 600.

"Barabara hii ina urefu wa kilomita 2.8 na tuliagizwa tujenge kwa kiwango cha changarawe na tumekamilisha kwa asilimia 100, hapa hii barabara ipo tayari kuanza kutumika kuanzia leo," alisema Masige.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliagiza Jeshi la Polisi na TANROADS kujadiliana ili kupanga magari yanayotakiwa kupita kwenye barabara hiyo ya mchepuko.

Alisema kama watakubaliana itumiwe na malori pekee basi magari mengine yaendelee kupita kwenye barabara kuu ili yasichangamane kwenye eneo hilo ambalo limekuwa hatari kwa maisha ya watu na vyombo vya usafiri. Homera aliwataka madereva kuheshimu taratibu zitakazokuwa zimewekwa pamoja na amri zitakazokuwa zinatolewa na maofisa wa Jeshi la Polisi watakaokuwa wanasimamia maeneo hayo.

"Kuanzia leo tunaizindua barabara hii ambayo itatumika kama njia ya muda mfupi kupunguza ajali ambazo zimekuwa zikitokea kwenye eneo hili, namwagiza RPC apange vizuri vijana wake kwenye maeneo haya ili magari yapite kwa utaratibu utakaokuwa umewekwa," alisema Homera.

Alisema ajali nyingi zimekuwa zikitokea katika eneo hilo kutokana na uzembe wa madereva ambao wamekuwa wakitumia gia kubwa ili kubana mafuta.

Hata hivyo alisema wakati hatua hizo za muda mfupi zikiendelea, serikali inaendelea na michakato ya kuchukua hatua za kudumu ikiwa ni pamoja na upanuzi wa barabara hiyo.





# Hemed awataka wadau wa elimu Unguja kushirikiana

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amewataka wadau wa elimu mkoa wa Kaskazini Unguja kushirikiana ili kuondosha tatizo la ufaulu mdogo wa wanafunzi wa mkoa huo.

Hemed alisema hayo jana wakati akizungumza na wazazi, walezi na walimu wakuu wa shule za maandalizi, msingi na sekondari za serikali na binafsi katika kikao cha kuimarisha utendaji kazi kilichofanyika Chuo cha Mafunzo ya Amali, Mkokotoni.

Alisema wazazi, walezi na walimu wakuu ndio wasimamizi wakuu wa wanafunzi na kwamba ushirikiano wao utawezesha kupata wataalamu bora ambao watalisaidia taifa baadaye. Hemed aliutaka uongozi wa mkoa wa Kaskazini Unguja kushirikiana na wizara kutumia mbinu mbadala ili kuondosha changamoto ya kufeli kwa wanafunzi.

"Kiujumla matokeo ya wanafunzi kwa mkoa wa Kaskazini hayako vizuri ukilinganisha na mikoa mingine. Lazima wazazi, walezi, walimu wakuu na vingozi wa mkoa tushirikiane ili kuondosha wimbi hili la kufeli kwa wanafunzi wetu kila mwaka," alisema.

Kuhusu uhamisho wa walimu, Hemed aliutaka uongozi wa mkoa kwa kushirikiana na wizara kukabiliana na tatizo hilo jambo ambalo linasababisha upungufu wa walimu na kushusha kiwango cha elimu.

Sambamba na hayo Makamu wa Pili wa Rais aliitaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha katika ajira zilizotangazwa kunakuwa na uwiano wa walimu kwa mujibu wa mahitaji halisi ili kuondosha tatizo la mrundikano wa walimu katika eneo moja na maeneo mengine kuendelea kuwa na uhaba.

"Serikali imeamua kuboresha maslahi kwa watumishi wake wakiwamo walimu ili kufanya kazi kwa weledi mkubwa na kuhakikisha wanapatikana wataalamu na viongozi bora wa hapo baadaye," alisema.

Pia alisisitiza haja ya wizara hiyo kufuatilia maendeleo ya walimu wa skuli zote za serikali na binafsi ili kuzalisha wataalamu wa kila sekta.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Khamis Ali Juma, alisema wizara imejipanga kutatua changamoto zinazowakabili walimu ikiwamo kulipwa feza zao hasa walimu waliotoka kwenye ugatuzi.

Aliwataka walimu wakuu, wazazi na walezi kuzisimamia kambi za wanafunzi zinazowekwa wakati wa kujiandaa na mitihani ya taifa ili kuepusha kuwa chanzo cha matatizo ya ukiukwaji wa maadili.

Kwa upande wao walimu wa shule za Mkoa wa Kaskazini Unguja waliomba serikali kuondosha changamoto zote zinazowakabili ikiwamo uchakavu wa majengo, ubovu wa barabara, uhaba wa vitendea kazi na kulipwa stahiki zao ili kufanya kazi kwa weledi kwa maslahi ya taifa.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman (kushoto), akibadilishana mawazo na Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, Machano Othman Said, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Chukwani, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Bil. 7/- kujenga barabara za lami Pemba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imetenga Sh. bilioni saba kwa ajili ya ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 13.5 inayokwenda moja kwa moja katika maeneo huru ya uchumi Micheweni, Pemba.

Hayo yamesemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, wakati akitoa ufafanuzi kuhusu mikakati ya serikali katika kukifungua kisiwa cha Pemba katika uwekezaji.

Alisema ujenzi wa barabara ya Micheweni inayokwenda katika maeneo huru ya Pemba ni miongoni mwa vipaumbele vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika uimarishaji wa miundombinu ya barabara.

Waziri aliitaja mikakati mengine ni kufikisha huduma za miundombinu ya umeme katika eneo la hekta 547 pamoja na maji safi na salama.

Alisema vipaumbele hivyo ni muhimu na ni sehemu ya mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar awamu ya nane ya kwenda kukifungua kisiwa cha Pemba katika uwekezaji wa miradi ya miundombinu.

Dk. Khalid alisema kazi hizo zinafanywa kwa pamoja kwa ushirikiano na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji ili kuhakikisha maeneo huru ya uwekezaji yanapata wawekezaji katika kisiwa cha Pemba.

"Mheshimiwa Spika napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba serikali imejipanga kuimarisha maeneo huru ya uchumi ya Micheweni kuona kwamba wawekezaji wanawekeza ambapo kwa upande wetu tutaimarisha miundombinu ya barabara," alisema.

Aidha alisema serikali imejipanga kujenga barabara yenye urefu wa kilomita 22.7 ambayo itaunganisha mikoa miwili ya Pemba katika miundombinu ya barabara hadi vijijini.

"Wizara imejipanga kutekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 22.7 ambayo inakwenda kuunganisha moja kwa moja mikoa miwili ya Pemba hatua ambayo ni mikakati ya kukifunguwa kisiwa hicho na sekta ya uwekezaji,' alisema.

Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka mkoa wa Kaskazini Pemba wakiongozwa na Mwakilishi wa Viti Maalumu, Bihindi Hamad Khamis, walitaka kupata ufafanuzi kuhusu mikakati ya serikali katika kuyaimarisha maeneo huru ya uchumi ya Micheweni Pemba ambayo uwekezaji wake bado haujaimarika hasa katika miundombinu.

# Kongamano TEHAMA kufanyika Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KONGAMANO la Sita la Kitaifa la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) linatarajiwa kufanyika Zanzibar Oktoba 26 hadi 28, mwaka huu.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari jana, kuhusu matayarisho ya kongamano hilo, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Dk Khalid Salum Mohamed, alisema kufanyika kwa kongamano hilo, Zanzibar itanufaika na fursa mbalimbali zitokanazo na mawasiliano ya teknolojia.

Alisema lengo la kongamano hilo ni kuwakutanisha wadau wa masuala ya TEHAMA duniani na kubadilishana uzoefu pamoja na ubunifu katika njia za kisasa za mawasiliano ili kukuza matumizi ya mawasiliano hayo.

Dk. Khalid alisema kupitia kongamano hilo kutakuwa na taarifa za utafiti mbalimbali, maonyesho ya TEHAMA, tunzo ya TEHAMA kwa wadau wenye mchango mkubwa katika teknolojia hiyo na kutatua vikwazo vinavyoikumba sekta ya mawasiliano nchini.

Pia alipongeza hatua zilizofikiwa za matumizi hayo ya TEHAMA lakini alisema bado kuna vikwazo vya taaluma kwa watendaji wa serikali na wananchi kwa ujumla na kwamba wamekuwa wakitafuta fursa mbalimbali za kukuza taaluma hizo hivyo kongamano hilo ni sehemu ya fursa katika kukuza uwelewa wa matumizi.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya TEHAMA, Dk. Nkundwe Mwansango, alisema kutokana na TEHAMA kugusa matumizi katika sekta mbalimbali, Zanzibar ina nafasi kubwa katika kukuza uwekezaji kupitia sekta kuu za uchumi ikiwamo utalii.

Alisema uwekezaji wa teknolojia ya mawasiliano Tanzania itaongeza uwekezaji hasa kwenye sekta ya uchumi wa bluu na kuchochea ajira mpya kupitia fursa hizo, hivyo kuinua uchumi na kukuza pato la taifa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**STELLA S. SUKA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.2769-0109** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ARI SEKONDARI mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/TAB/RB/361686/2022.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SHAMILA S. RAMADHAN** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.2769-0104** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ARI SEKONDARI mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/TAB/RB/361684/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DAYOSISI YA KUSINI KATI-IDARA YA UDIAKONIA** inatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **ISUZU BUS** yenye usajili namba **T575 DJL.** CHASSIS NAMBA: **CVR70K3000557.** ENGINE NAMBA: **8PDIEAA0551.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **MKT/RB/413/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AFRICA PROPER EDUCATION NETWORK** inatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 214 DEP – NISSAN CARAVAN.** Chassis namba **VPE25072709.** Engine namba **KA20068439X.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Control **No: 9910833889928.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SULEIMAN MOHAMED SULEIMAN** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 390 AVR – SUZUKI ESCUDO.** Chassis namba **JSAFHX5150107041.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **KW/RB/4313/2022.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 131 OF 2022**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE LUDWINA SEVERINE MSAKI**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY FADHILI ALLY KASIRA**

**GENERAL CITATION**
**( Rule 75 of Probate Rules)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 5 Day of 10.....................2022
Dated at Dodoma this 3rd day of September 2022

**PETITIONER**
Presented for filing this......15...day of......9...........2022

MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE ... DODOMA DISTRICT

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya...Tabora**

**Kituo cha.... Isevya Mkoa.... Tabora**

**Usimamizi wa Mirathi Na 67/ 2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**

**Marehemu Absalom Yesaya wa Mtendeni-Tabora**

**Katika shauri la maombi ya kumteua msimamizi yaliyoletwa Na James Absalom Kapalala**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5 (2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu.
Wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 5 mwezi 10, 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia; Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuleta mahakamani kukaguliwa.

**Imetolewa tarehe 14/09/2022**


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

***Uza,***
***Chenye Thamani***
***Kubwa Kwa***
***Kutangaza Nasi Kwa***
***Bei Poa***
***Tupigie, 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe





TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Maelfu wajitokeza kuaga mwili wa Malkia Elizabeth

**LONDON, Uingereza**

MAELFU ya waombolezaji kutoka matabaka mbalimbali nchini Uingereza, wamejitokeza kuuaga mwili wa Malkia Elizabeth katika ukumbi wa Westminster mjini London.

Jeneza la Malkia huyo aliyeongoza kwa miongo saba litakaa ukumbini hapo kwa siku nne kabla ya mazishi yake yatakayofanyika Jumatatu wiki ijayo.

Baada ya siku kadhaa za kupitishwa katika maeneo mbalimbali na kufanywa taratibu za Kifalme wakati mwili wa malkia huyo ukiletwa mjini London kutoka kasri ya Balmoral nchini Scotland, ambako alifariki dunia Alhamisi iliyopita akiwa na umri wa miaka 96.

Maofisa wanatarajia kuwa karibu watu 750,000 watajitokeza kuaga mwili wa Malkia huyo kabla ya kuzikwa.

**DW**

## Abiria mwingine wa Kenya Airways afariki

**NAIROBI, Kenya**

SHIRIKA la ndege la Kenya Airways limethibitisha kuwa abiria mmoja alipata matatizo ya kupumua alipokuwa akipanda moja ya ndege zake na kisha kufariki dunia.

Katika taarifa iliyotolewa juzi, KQ ilisema abiria huyo alitangazwa kufariki katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta (JKIA) huku ndege hiyo iliyokuwa ikielekea Mombasa ikiwa bado ardhini.

“Kenya Airways PLC inasikitika kutangaza kwamba abiria alipata matatizo ya kupumua jioni hii alipokuwa akipanda KQ612 ambayo iliratibiwa kuondoka hadi Mombasa saa 19: 00,” ilisema taarifa hiyo.

“Abiria huyo alitangazwa kuwa amefariki na wafanyikazi wa matibabu katika JKIA wakati ndege ilikuwa ingali chini,” KQ iliongeza katika taarifa yake.

Shirika hilo mapema mwezi huu lilithibitisha abiria mwingine aliyekuwa kwenye mojawapo ya safari zake za ndege kuelekea New York kutoka Nairobi alikuwa ameaga dunia, ikiwa ni tukio la pili kama hilo kuripotiwa katika muda wa siku tisa.

Mwezi uliopita, iliripotiwa tukio lingine ambapo abiria alifariki kwenye mojawapo ya ndege zake kutoka New York kuelekea Nairobi.

Kulingana na shirika hilo la ndege, abiria huyo alipata matatizo ya kupumua saa saba baada ya ndege hiyo kupaa kutoka New York kabla ya kufariki.

Msemaji wa familia alisema alikuwa na historia ya ugonjwa wa kisukari.

**BBC**

# Azerbaijan, Armenia zasitisha mapigano

**YEREVAN, Armenia**

NCHI za Azerbaijan na Armenia zimetangaza kusitisha mapigano baada ya kukabiliana kwa siku mbili.

Taarifa kuhusu makubaliano hayo imetolewa na Katibu wa Baraza la Usalama wa Taifa nchini Armenia, Armen Grigoryan, ambaye alisema usitishaji wa mapigano umeanza kutekelezwa usiku wa kuamkia jana.

Muda mfupi baada ya tangazo hilo, Wizara ya Ulinzi ya Armenia ilithibitisha kwamba mashambulizi kutoka upande wa Azerbaijan yamesitishwa, licha ya kuwa nchi hiyo haijazungumzia chochote juu mwafaka uliopatikana.

Jumla ya wanajeshi 155 kutoka pande zote mbili wameuwawa katika mapigano hayo.

Armenia ndiyo imepoteza idadi kubwa ya wapiganaji wake.

Takwimu za vifo kwa upande wa Armenia zimetolewa na waziri mkuu wa nchi hiyo Nikol Pashinyan aliyesema wanajeshi 105 wameuwawa.

Hata hivyo, idadi kubwa ya wanajeshi waliouwa inaweza kuzidisha hasira miongoni mwa raia nchini Armenia.

Juzi maelfu ya Waarmenia waliingia mitaani kuandamana dhidi ya utawala wa waziri mkuu Pashiyan wakimtuhumu kuisaliti nchi hiyo ili kuiridhisha Azerbaijan.

Wengi walibeba ujumbe wa kumtaka Pashinyan ajiuzulu.

Waziri mkuu huyo mbali na kutoa taarifa ya idadi ya wanajeshi waliouwawa, aliarifu pia kwamba Azerbaijan imenyakua eneo la ardhi ya Armenia lenye ukubwa wa kilometa 10 za mraba tangu mapigano yalipozuka mwanzoni mwa wiki.

Aliwaambia wabunge mjini Yerevan kuwa serikali yake imeomba msaada wa kijeshi kutoka Russia chini ya mkataba wa ushirikiano baina ya nchi hizo mbili na ushirika wa kiusalama kati ya mataifa sita yaliyokuwa sehemu ya Muungano wa Kisovieti.

Kwa miongo miwili Armenia na Azerbaijan zimekuwa kwenye uhasama juu ya masuala ya mipaka unaochochewa kwa sehemu kubwa na mapambano ya kuwania udhibiti wa jimbo la Nagorno Karabakh.

Jimbo hilo ambalo kihistoria lina wakazi wengi wa jamii ya Armenia linatambulika kisheria kuwa ni sehemu ya Azerbaijan tangu enzi ya Dola ya Kisovieti, ambayo mataifa yote hayo mawili yalikuwa sehemu ya dola hiyo.

***DW***



Mfalme Charles wa Uingereza akiambatana na familia yake ya kifalme William, Sir Timothy Laurence, Harry, Peter Phillips, Anne, wakati wakisindikiza jeneza la Malkia Elizabeth kwa ajili ya kuagwa na raia wa nchi hiyo jijini London. **PICHA: REUTERS**

# Russia yalipua bwawa la maji Ukraine

**KYIV, Ukraine**

RAIS wa Ukraine Volodymyr Zelensky, amesema kwamba shambulio la kombora kwenye bwawa la Krivoy Rog halitavunja ari ya wanajeshi wa nchi yake.

“Waligundua kuwa amri ya Russia ni ya wastani, na kwamba wanatarajiwa kushindwa nchini Ukraine katika pande zote. Russia haitarekebisha hili kwa ugaidi wowote, kwa sababu ugaidi unathibitisha tu udhaifu wa yule anayetekeleza,” alisema Zelensky katika hotuba yake ya kila siku jioni.

Kulingana na kiongozi huyo, njia pekee ya askari wa Russia kusalimika ni kujisalimisha kwa wanajeshi wa Ukraine, kwani itashindwa vita.

‘‘Atapoteza sio tu vita hivi , lakini historia yenyewe huandikwa na binadamu. Wale wote waliotushambulia kwa makombora. Wale waliovamia ardhi yetu, waoga. Ninyi ni watu walio na udhoofu ambao baada ya kutoroka katika mstari wa mbele wa vita mnajaribu kufanya uhalifu kutoka mbali”, alisema rais huyo wa Ukraine.

Makombora ya Russia yalipiga bwawa la akiba ya maji lililopo katika mji wa kusini mwa Ukraine wa Kyiv Rih.

Kulingana na mkuu wa mji huo Oleksandr Vilkul, alisema wakazi katika baadhi ya maeneo walitakiwa kuondoka.

Hata hivyo, alisema kuwa shambulio hilo lilikuwa ni kisasi cha shambulizi lake la hivi karibuni la kukabiliana nao.

Rais Volodymyr Zelensky ambaye alizaliwa katika mji huo aliielezea Russia kama taifa la kigaidi muda mfupi baada ya shambulio katika bwawa la Karachunivske.

Katika hotuba yake hiyo Zelensky alisema bwawa lilikuwa halina thamani ya kijeshi kabisa.

Vilkul alisema usiku kulisikika milipuko miwili na kulipua bwawa hilo na kuongezeka mtiririko wa maji kuelekea kwenye mto Inhulets.

Usambazaji wa maji katika mji huo uliathiriwa na shambulio, ambalo lilitumiwa na watu zaidi ya 600,000 kabla ya vita.

***BBC***

# KIPANGA YAJIPANGA KUWEKA REKODI MPYA MICHUANO CAF

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KATIKA kuhakikisha inasonga mbele katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Kocha Msaidizi wa Kipanga FC, Hassan Abdulrahman, amesema kikosi chake kimejipanga kupambana na hatimaye kupata ushindi katika mechi ya marudiano dhidi ya Al Hilal Wau kutoka Sudan Kusini.

Mabingwa hao wa Kombe la Shirikisho, Kipanga wanatarajia kuwakaribisha Wasudani hao kesho kwenye Uwanja wa Amaan, visiwani hapo.

Katika mechi ya kwanza iliyochezwa wiki iliyopita kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, timu hizo ziltoka sare ya bao 1-1.

Akizungumza na gazeti hili jana, Abdulrahman alisema, wanaendelea kurekebisha makosa yaliyojitokeza katika mechi ya kwanza ili kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kupata ushindi na hatimaye kusonga mbele katika michuano hiyo.

Kocha huyo alisema wachezaji wao wote wako katika ari nzuri na wamedhamiria kuweka rekodi ya kufika mbali katika mashindano hayo yanayofanyika kila mwaka chini ya usimamizi wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

"Jumamosi tutakuwa nyumbani katika dimba la Amaan kusaka kupata alama muhimu zitakazotupa njia ya kusonga mbele katika michuano hiyo ya kimataifa ya Afrika, tunaamini tutafikia malengo, mwaka huu tumedhamiria kupeperusha vyema bendera ya Zanzibar," kocha huyo alisema.

Aliongeza wanatarajia kutumia faida ya uwanja wa nyumbani kuwabana wapinzani wao na kutimiza mipango yao ya kuvuka hatua hiyo ya awali.

"Mpaka sasa kikosi chetu kipo salama na kinaendelea vizuri na programu zake za mazoezi, tupo tayari kwa mchezo huo wa marudiano tukiwa kwenye dimba la nyumbani tulilolizoea," Abdulrahman alisema.

Aliongeza hana majeruhi hata mmoja katika kikosi hicho huku akieleza anajivunia kutumia wachezaji wazawa pekee. "Ninajua tutacheza na timu ambayo ina uzoefu, wao pia wataingia uwanjani wakiwa na malengo ya kupata matokeo mazuri ili kuvuka hatua hii kama ilivyo kwa upande, tunamwomba Mungu iwe bahati ya Kipanga siku ya Jumamosi," aliongeza.

Aliwaomba mashabiki wa timu hiyo kujitokeza kwa wingi ili kuhakikisha wanawaongezea morali wachezaji wakati wote wa mchezo.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Vijana ya Taifa ya umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Black Rhino ulioko Karatu mkoani Manyara kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-17), yatakayofanyika hivi karibuni nchini Ethiopia. **PICHA: TFF**

# DAWASA yaanza vyema Maji CUP

**Na Mwandishi Wetu, MOROGORO**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imeanza vyema mashindano ya Kombe la Maji (Maji Cup), kwa kuwafunga wenzao kutoka Tabora (TABORA WSSA) mabao 3-0 katika mchezo wa michuano hiyo uliochezwa kwenye Uwanja wa Kampasi Kuu ya SUA, Morogoro.

Huu ni msimu wa pili wa michuano hiyo inayoendelea mkoani Morogoro.

DAWASA iliyoonyesha soka safi na kuvutia mashabiki wengi waliokuwa uwanjani hapo na ilipata ushindi huo kupitia kwa wachezaji wake, Patrick Ntuli aliyefunga goli moja na nahodha wa timu hiyo, Prosper Nyagawa aliyefunga mabao mawili.

Akizungumza baada ya mchezo huo kumalizika, Kocha Mkuu wa DAWASA, Mohamed Magali, alisema siri ya mafanikio ya ushindi huo ni ushirikiano mkubwa waliopata kutoka kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja, pamoja maandalizi mazuri waliyoyafanya kuelekea mashindano hayo.

"Wachezaji wamepambana na kuonyesha kupigania nembo ya mamlaka, tumeishi katika kauli ya Mamlaka kufanya kazi kwa viwango na ubora na wachezaji wamehamishia hayo katika kiwanja," alisema Magali.

DAWASA itashuka dimbani tena Jumanne kuwakabili Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Mkoa wa Lindi.

## KMC FC macho yote kwa Ihefu

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa KMC FC, Thierry Hitimana, amesema kikosi chake kimeendelea kuimarika kuelekea mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ihefu utakaochezwa Septemba 21, mwaka huu kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Hitimana alisema wachezaji wake wanaendelea vizuri na mazoezi na kila mmoja anaonyesha ushindani kwa kuwania namba katika kikosi cha kwanza.

"Tunatarajia mechi itakuwa ngumu kwa sababu Ihefu imepoteza mechi zote tatu zilizopita, hatutawadharau, tutaingia uwanjani kwa tahadhari," Hitimana alisema.

Naye Msemaji wa KMC, Christina Mwagala, alisema ili kujiweka tayari na mechi hiyo, leo wanatarajia kucheza mchezo wa kirafiki kwa lengo la kuwajenga wachezaji wake.

"Kesho (leo) tutakuwa na mchezo wa kirafiki na tunatarajia kucheza na timu inayoshiriki Ligi Kuu, tutawafahamisha timu tutakayocheza nayo ikifika jioni," alisema Mwagala.

Mchezo uliopita KMC ililazimisha sare ya mabao 2-2 dhidi ya Simba.

## Ahmadiyya Cup mambo yameiva

**Na Isiyaka Nyamihasi,TUDARCo**

TIMU ya Shule ya Sekondari ya Ahmadiyya inatarajia kukutana na Upendo FC katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la Ahmadiyya itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Msongora, Dar es Salaam.

Kocha wa Ahmadiyya, Khalid Adam, alisema timu yake imejiandaa vizuri ingawa amejipanga kukutana na ushindani kwenye hatua hiyo.

"Tuna maono ya mbali hasa pale tunapohitaji kuinua na kukuza vipaji vya wachezaji, ninahisi tutakutana na changamoto zaidi katika hatua zinazofata," alisema Adam.

Naye Kocha wa Mbande FC ambaye timu yake itakutana na Msongola Veterans katika mechi ya nusu fainali ya pili itakayochezwa keshokutwa, Tombi Revocatus, alisema amewaandaa vyema vijana wake na wana uchu wa kuchukua ubingwa wa mashindano hayo.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano hayo, Mohamedi Ngunde, alisema michuano hiyo itafikia tamati ifikapo Septemba 25, mwaka huu.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**OBLACK KUMRITHI DE GEA**

KLABU ya Manchester United inamtaka mlinda mlango wa Atletico Madrid na Timu ya Taifa ya Slovenia, Jan Oblak mwenye umri wa miaka 29, kuchukua nafasi ya David de Gea. ***(Jeunes Footuex)***

**CITY, CHELSEA VITANI**

MANCHESTER City inajiandaa kuungana na Chelsea katika mbio za kumnunua mshambuliaji wa AC Milan na Timu ya Taifa ya Ureno, Rafael Leao mwenye umri wa miaka 23. ***(Calciomercato)***

**CHELSEA ILIMTAKA LEAO**

CHELSEA ilituma ofa isiyo rasmi kwa Rafael Leao katika dirisha la usajili la majira ya kiangazi, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Milan, Paolo Maldini. ***(Sky Sports via SempreMilan.it)***

**ORIGI KUONDOKA MILAN**

AC Milan wanatafuta mbadala wa mshambuliaji wa Ubelgiji, Divock Origi, licha ya kumsajili tu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 msimu huu wa joto. ***(Calciomercato)***

**HAALAND ALITAJWA UNITED**

OLE Gunnar Solskjaer alipendekeza mshambuliaji, Erling Haaland kutua Manchester United wakati wote wawili walikuwa katika klabu ya Norway ya Molde, lakini Mashetani Wekundu hao hawakuonyesha nia ya kumhitaji. ***(Athletic)***

**JAMES HUYO UGIRIKI**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Everton na Real Madrid, James Rodriguez mwenye umri wa miaka 31, amekamilisha vipimo vya afya kabla ya kuhamia Ugiriki kujiunga na klabu ya Olympiakos. ***(Fabrizio Romano)***

**KUOL KUTUA NEWCASTLE**

KLABU ya Newcastle imekubaliana na mshambuliaji mzaliwa wa Misri, Garang Kuol, mwenye umri wa miaka 18, ambaye anachezea Australia katika klabu ya Central Coast Mariners. ***(BeIn Sports)***

**COSTA DIMBANI ENGLAND**

MSHAMBULIAJI mpya wa Wolves, Diego Costa mwenye umri wa miaka 33, ana nafasi ya kucheza mechi yake ya kwanza katika klabu hiyo katika mchezo wao dhidi ya Manchester City utakaofanyika kesho baada ya mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Hispania kushiriki katika mazoezi kamili. ***(Mail)***

**MELO NJIA MOJA**

LIVERPOOL haitasita kusitisha mkataba wa mkopo wa Arthur Melo kutoka Juventus iwapo watamtambua kiungo atakayechukua nafasi ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 26, katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Tuttomercato)***

**SVENSSON KUMRITHI POTTER**

KLABU ya Brighton imemtambua Kocha Mkuu wa Mainz, Bo Svensson kama mbadala wa Graham Potter. ***(Athletic)***

**CHELSEA KUTUA URENO**

CHELSEA imekuwa ikifanya mazungumzo kuhusu kununua klabu nchini Ureno kama sehemu ya mpango wa Mwenyekiti wao, Todd Boehly wa kumiliki vilabu vingi duniani. ***(Telegraph)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# POTTER ATARAJIA MAZURI CHELSEA

●●● Kocha huyo mpya asema kikosi chake kitaimarika baada ya...

**LONDON, England**

KOCHA Mkuu wa Chelsea, Graham Potter ameapa Chelsea "itaimarika" mara watakapofanyia kazi mambo madogo madogo baada ya kutoa sare ya bao 1-1 dhidi ya Red Salzburg katika mchezo wake wa kwanza tangu akabidhiwe timu hiyo.

Mchezo huo ulikuwa wa pili kwa Chelsea kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambao ulichezwa juzi.

Chelsea walitangulia kupata bao kupitia Raheem Sterling dakika 48 na hilo ndilo lilikuwa jaribio lao la kwanza kulenga lango.

Hata hivyo, The Blues walifanya majaribio mengi ya kutaka kupata mabao zaidi na ndipo wakarudishwa nyuma dakika 15 kabla ya mchezo kumalizika wakati Noah Okofar aliposawazisha kutokana na makosa ya Thiago Silva.

Kikosi cha Potter kilimalizika mchezo huo pale Stamford Bridge na asilimia ya 72 ya umiliki wa mpira na walikuwa na mashuti 17, lakini ni manne kati ya hayo pekee yaliyolenga lango.

Lakini licha ya sare hiyo walioipata Potter alifurahishwa na jinsi wachezaji wake walivyojituma uwanjani.

"Tumesikitishwa na matokeo. Nilidhani wachezaji walitoa kila kitu," aliambia BT Sport .

"Tulifunga bao zuri lakini tulipoteza kidogo kipindi cha pili. Kipa wao ameokoa vyema, ndivyo ilivyo, lazima tujitafute wenyewe."

Potter aliongezea kwa kusema siku zote kuruhusu bao kunakera na safu ya ulinzi ilikuwa bora kwa ujumla ni maeneo madogo tu ambayo yanatakiwa kuboreshwa.

Chelsea mechi ya kwanza alichapwa bao 1-0 na Dinamo Zagreb na ndio mechi iliyomfukuzisha Thomas Tuchel, na sasa baada ya kutoa sare anakuwa na alama moja kwenye kundi ambalo anashika mkia huku kinara wa kundi hilo akiwa AC Milan mwenye pointi nne.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,031,2

MECHI KALI
RUVU SHOOTING
VERSUS
POLISI TANZANIA
1 | 2.14
X | 2.74
2 | 3.72

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa, vodacom m-pesa, airtel money, ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# JOSHUA NA TYSON KUZICHAPA DESEMBA

**LONDON, England**

BONDIA Anthony Joshua amekubali masharti ya bingwa wa WBC, Tyson Fury kwa ajili ya pambano la uzito wa juu linalowakutanisha Waingereza hao litakalofanyika Desemba 3, mwaka huu.

Kampuni inayomsimamia bondia huyo, 258MGT inasema kwa sasa "anasubiri majibu", rasmi.

Joshua mwenye umri wa miaka 32, alipewa ofa na timu ya Fury, ambaye alipendekeza pambano hilo kufanyika siku hiyo na mgao wa asilimia 60 kwa 40.

Makubaliano ya pambano yalifikiwa siku ya Ijumaa lakini tangazo lilicheleweshwa kutolewa kwa sababu ya kifo cha Malkia Elizabeth II kilichotokea Alhamisi iliyopita.

Masharti ya awali yamekubaliwa lakini Joshua bado hajasaini mkataba.

Katika taarifa iliyotumwa kwenye mtandao wa Twitter ilisema: "258 na Matchroom Boxing wanaweza kuthibitisha, kwa niaba ya Anthony Joshua, tumekubaliana na masharti yote yaliyowasilishwa kwetu na timu ya Fury kwa ajili ya pambano hilo."

Fury mwenye umri wa miaka 34, alisema angestaafu baada ya kumpiga, Dillian Whyte Aprili, mwaka huu na akarudia madai hayo mwezi uliopita.

Uwanja wa Timu ya Cardiff, Principality unapigiwa chapuo, huku Saudi Arabia au nchi nyingine ya Mashariki ya Kati pia inaweza kuwa mwenyeji wa pambano hilo.

# James atua Olympiacos

**LONDON, England**

JAMES Rodriguez, mchezaji wa zamani wa Real Madrid anakaribia kujiunga na klabu ya Olympiacos ya nchini Ugiriki.

James ambaye alikuwa anaitumikia Al- Rayyan ya Qatar amefanya mazungumzo na klabu hiyo kongwe ya nchini Ugiriki na yupo kwenye hatua za mwisho za kujiunga nao.

Mchezaji huyo amesafiri kuelekea Ugiriki kukamilisha vipimo vya afya ili kujiunga na klabu hiyo kwa sababu tayari makubaliano binafsi yameshafikiwa baina ya klabu na mchezaji huyo.

Nyota huyo wa zamani wa klabu za Porto, As Monaco, Real Madrid, Bayern Munich pamoja na Everton amekua hana wakati mzuri tangu aondoke Santiago Barnabeu na amezunguka klabu kadhaa ndani na nje ya Ulaya.

Nyota huyo wa kimataifa wa Colombia anakwenda kuungana na nyota mwenzake wa zamani wa Real Madrid, Marcelo Viera ambaye naye amejiunga na timu hiyo hivi karibuni.

43,893/-

# WALIOVAMIA UWANJA WA SIMBA WAPEWA SIKU 60

**Na Jenifer Gilla**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amewapa siku 60 wakazi tisa waliovamia katika eneo la Uwanja unaomilikiwa na Klabu ya Simba ya jijini maarufu kwa jina la Mo Simba Arena uliopo Bunju kuhama mara moja.

Makalla pia ameruhusu klabu hiyo kuendelea na mradi wa ujenzi wa ukuta kuzunguka eneo la uwanja huo ambao ulisimama kwa ajili ya uvamizi huo.

Bosi huyo wa Dar es Salaam alisema hayo alipokuwa katika ziara ya kutembelea eneo hilo na kukagua wananchi waliovamia akiongozana na Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe pamoja na viongozi wa klabu hiyo kongwe hapa nchini.

"Kiwanja ama eneo, kama huna hati, wewe ni mhalifu kama alivyo mhalifu mwingine yoyote yule, katika jicho la sheria. Huo ndio msingi wake, kama huna karatasi lolote, unavunja sheria ya nchi.

"Mwenyekiti nimeona muhtasari wenu mliokaa kikao cha Novemba, mwaka jana, mnakiri kabisa watu wako wamevamia, kwa nini hamwondoki? Halafu wala hamna maendeleo makubwa," alihoji Makalla.

Aliongeza Simba walipewa eneo hilo na Rais Mstaafu, Jakaya Kikwete ili wajenge uwanja na wawe sehemu yao kama klabu na uamuzi huo unatakiwa uheshimiwe.

Naye Gondwe alisema wanatii agizo la Makalla la kuwapa haki wenye hati halali katika eneo lililovamiwa hata kama wasiokuwa na hati watakuwa ni wengi.

"Kwa sababu tukiendelea kutowapa haki wenye hati ina maana hati za serikali zitakuwa hazina maana katika umiliki ambao mtu huyo anapewa na serikali," alisema Gondwe.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema walitumia busara ya kuwapa muda wakazi hao ili wahame katika eneo hilo lakini anashangaa kuona bado wanaendelea kuwapo.

"Simba tunataka kuendeleza kile ambacho tuliahidi kwa wananchi wetu,tunataka kutimiza wajibu wetu kama tulivyoahidi mwezi wa sita," alisema Barbara.



Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni ,Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas (katikati), akizungumza na wajumbe kutoka sehemu mbalimbali katika kikao cha maandalizi ya Tamasha la Muziki litakalofanyika hivi karibuni hapa nchini. **PICHA: MTANDAO**

# Bodi ya Ligi yawachana waamuzi

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), imesema baadhi ya waamuzi wanakosa ujasiri, kuwasiliana, mwendelezo na kutumia akili ya kuzaliwa wanapochezesha mechi mbalimbali hapa nchini na ofisi yake inawakumbusha ili mwamuzi awe bora ni lazima awe na vitu hivyo, imefahamika.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam na Kamati ya Waamuzi, Ofisa Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almasi Kasongo, alisema kumekuwa na malalamiko mengi kwa waamuzi lakini ikifuatiliwa inagundulika baadhi wanakosa sifa hizo alizozitaja.

"Mwamuzi ni kama hakimu au jaji, ni lazima kwanza uwe jasiri, na mwamuzi mzuri anapimwa kwa vitu kama hivyo.

"Kuna baadhi ya waamuzi wamekariri penalti haitoki dakika ya 94, au dakika ya kwanza, huko ni kukosa ujasiri, penalti inatoka dakika yoyote ile hata dakika ya 97 na kadi nyekundu inatoka muda wowote ule na anaonyeshwa yoyote yule," alisema Kasongo.

Aliongeza makosa ambayo ya waamuzi lakini wakitazama msingi wake ni kutokuwa na mawasiliano tu baina yao, huku sifa nyingine akiitaja ni kutumia akili ya kuzaliwa.

"Katika vikao vya kamati hakuna timu ambayo haijapigwa faini kwa mashabiki wake kurusha chupa na mawe, tumefuatilia msingi wake, imegundulika kuwa waamuzi wanakosa mwendelezo mzuri wa uchezeshaji na maamuzi," aliongeza bosi huyo.


SUPA JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 17/09/22 | 18:00 | Montpellier vs Strasbourg | 2.73 | 3.33 | 2.48 |
| 02. 17/09/22 | 19:00 | Spezia vs Sampdoria | 2.55 | 3.25 | 2.75 |
| 03. 17/09/22 | 19:15 | Zulte Waregem vs St. Truiden | 2.94 | 3.49 | 2.28 |
| 04. 17/09/22 | 19:30 | Valencia vs Celta Vigo | 2.35 | 3.08 | 3.18 |
| 05. 17/09/22 | 19:30 | Borussia Monchengladbach vs RB Leipzig | 2.93 | 3.57 | 2.23 |
| 06. 17/09/22 | 20:00 | PAU F vs Valenciennes | 2.72 | 3.07 | 2.77 |
| 07. 17/09/22 | 20:00 | Bastia vs Metz | 2.52 | 3.17 | 2.92 |
| 08. 17/09/22 | 20:00 | US Quevilly Rouen vs Laval | 2.47 | 3.16 | 3.01 |
| 09. 17/09/22 | 22:30 | Atlanta United vs Philadelphia Union | 2.30 | 3.61 | 2.91 |
| 10. 18/09/22 | 02:30 | New England Revolution vs Montreal Impact | 2.35 | 3.57 | 2.87 |
| 11. 18/09/22 | 13:15 | GO Ahead Eagles vs FC Emmen | 2.36 | 3.48 | 2.83 |
| 12. 18/09/22 | 14:30 | Jahn Regensburg vs St. Pauli | 2.88 | 3.62 | 2.26 |
| 13. 18/09/22 | 15:00 | Randers FC vs Silkeborg IF | 2.47 | 3.39 | 2.74 |
| 14. 18/09/22 | 15:30 | SC Heerenveen vs Twente | 2.73 | 3.58 | 2.38 |
| 15. 18/09/22 | 16:00 | Clermont Foot vs Troyes | 2.40 | 3.33 | 2.83 |
| 16. 18/09/22 | 17:30 | FC Arouca vs Vitoria Guimaraes | 2.79 | 3.19 | 2.54 |
| 17. 18/09/22 | 19:00 | FC Midtjylland vs FC Copenhagen | 2.50 | 3.40 | 2.70 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 16/09/2022


| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 5633 | Sagan Tosu vs Kashima Antlers | 2.89 | 3.23 | 2.25 |
| 16:00 | 3159 | Ruvu Shooting vs Polisi Tanzania | 2.14 | 2.74 | 3.72 |
| 16:00 | 5108 | Cape Town All Stars vs Polokwane City | 2.02 | 3.14 | 3.48 |
| 18:00 | 2110 | Voluntari vs U Craiova SA | 2.90 | 3.00 | 2.50 |
| 18:00 | 3469 | FC Riga vs FK Liepaja | 1.54 | 3.94 | 5.12 |
| 18:20 | 3764 | AL Arabi vs AL Tadamon | 1.54 | 3.94 | 5.12 |
| 18:30 | 4788 | MC Alger vs MC Magra | 1.52 | 3.62 | 6.07 |
| 18:50 | 5098 | Al Taawon vs Dhamk | 1.66 | 3.84 | 4.85 |
| 19:00 | 5550 | GKS Piast Gliwice vs Slask Wroclaw | 1.79 | 3.43 | 4.02 |
| 19:00 | 5985 | Vitebsk vs BATE Borisov | 4.61 | 3.44 | 1.69 |
| 19:10 | 1929 | SV Horn vs First Vienna | 2.36 | 3.25 | 2.71 |
| 19:30 | 1348 | Fremad Amager vs HB Koge | 3.24 | 3.54 | 1.97 |
| 19:30 | 1714 | Sandhausen vs Hannover | 2.95 | 3.30 | 2.29 |
| 20:00 | 2539 | Hatayspor vs Kayserispor | 2.22 | 3.31 | 3.11 |
| 20:00 | 4633 | Galatasaray vs Konyaspor | 1.71 | 3.71 | 4.51 |
| 20:00 | 4645 | FC Helsingor vs Naestved BK | 1.75 | 3.65 | 3.95 |
| 20:00 | 4702 | Horsens vs Nordsjalland | 3.01 | 3.42 | 2.22 |
| 20:00 | 5166 | Tondela vs Belenenses | 1.93 | 3.28 | 3.83 |
| 20:00 | 5612 | Yeni Malatyaspor vs Altay | 2.70 | 3.24 | 2.37 |
| 20:30 | 1541 | Nancy vs Bastia Borgo | 1.74 | 3.53 | 4.38 |
| 20:30 | 1560 | Avranches vs Red Star | 3.03 | 3.33 | 2.20 |
| 20:30 | 3148 | Neuchatel Xamax vs FC Thun | 4.12 | 3.58 | 1.73 |
| 20:30 | 3421 | Dunkerque vs Cholet | 1.63 | 3.70 | 4.99 |
| 20:30 | 4727 | Bourg Peronnas vs Saint Brieuc | 1.83 | 3.53 | 3.93 |
| 21:00 | 2466 | Helmond Sport vs Dordrecht | 1.88 | 3.59 | 3.64 |
| 21:00 | 3708 | Maastricht vs Jong Ajax | 3.19 | 3.94 | 1.93 |
| 21:00 | 4188 | De Graafschap vs Almere City | 1.78 | 3.69 | 3.99 |
| 21:00 | 4453 | Utrecht vs NEC Nijmegen | 1.70 | 3.80 | 4.39 |
| 21:00 | 4577 | PEC Zwolle vs ADO Den Haag | 1.48 | 4.47 | 5.37 |
| 21:00 | 5483 | Al Hilal Riyadh vs Al Wehda | 1.06 | 13.00 | 17.00 |
| 21:00 | 5487 | FC Eindhoven vs Roda Kerkrade | 2.44 | 3.29 | 2.69 |
| 21:00 | 5574 | VVV Venlo vs Jong PSV | 2.16 | 3.58 | 2.93 |
| 21:00 | 5680 | Telstar vs Heracles Almelo | 4.09 | 3.69 | 1.76 |
| 21:30 | 3834 | Mainz vs Hertha BSC | 1.65 | 3.91 | 4.62 |
| 21:30 | 4737 | Brescia vs Benevento | 2.12 | 3.29 | 3.29 |
| 21:30 | 5430 | Legia Warszawa vs Miedz Legnica | 1.57 | 3.87 | 4.90 |
| 21:45 | 1596 | Newry City AFC vs Dungannon Swifts | 2.03 | 3.59 | 3.05 |
| 21:45 | 1691 | Cobh Ramblers vs Athlone Town | 1.99 | 3.63 | 3.09 |
| 21:45 | 2263 | Crusaders Belfast vs Linfield Belfast | 3.00 | 3.45 | 2.10 |
| 21:45 | 2975 | Waterford Utd vs Dundalk FC | 6.68 | 4.71 | 1.35 |
| 21:45 | 3417 | Royal Antwerp vs RFC Seraing | 1.31 | 5.23 | 8.44 |
| 21:45 | 3703 | Galway United vs Cork City | 2.46 | 3.24 | 2.60 |
| 21:45 | 3931 | Salernitana vs Lecce | 2.09 | 3.30 | 3.35 |
| 21:45 | 4439 | Treaty United vs UCD Dublin | 2.64 | 3.47 | 2.31 |
| 22:00 | 1050 | Valladolid vs Cadiz CF | 2.03 | 3.22 | 3.73 |
| 22:00 | 1157 | Levante vs FC Cartagena | 1.63 | 3.76 | 5.02 |
| 22:00 | 1338 | Aston Villa vs Southampton | 2.01 | 3.46 | 3.41 |
| 22:00 | 3098 | Nottingham vs Fulham | 2.70 | 3.24 | 2.50 |
| 22:00 | 4171 | AJ Auxerre vs Lorient | 2.66 | 3.26 | 2.56 |
| 22:15 | 1511 | Portimonense vs GD Chaves | 2.15 | 3.16 | 3.41 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Ijumaa Septemba 16, 2022

Nipashe



Joshua, Tyson kuzichapa Desemba UKURASA 22



Wachezaji wa Yanga, Stephanie Aziz Ki (kushoto) na Mkongomani, Heritier Makambo (kulia) wakifurahia baada ya nyota huyo raia wa Burkina Faso kufunga bao lake la kwanza tangu alipojiunga na klabu hiyo walipoikabili Mtibwa Sugar katika mechi ya Ligi Kuu Bara mapema wiki hii. **PICHA: MTANDAO**

## Mastraika Yanga watafutiwa dawa

**Na Saada Akida**

TUNAANZA upya, hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi, kuelekea mechi ya marudiano ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Zalan FC kutoka Sudan Kusini itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Nabi alisema anawataka wachezaji wake wajitathmini ubora wao kwa sababu ya ushindani uliopo mbele yao katika Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano hayo ya kimataifa wanayoshiriki.

Nabi alisema mchezo wa kesho hautakuwa rahisi hivyo anawakumbusha wachezaji kufanyia kazi maelekezo yote anayowapa wanapokuwa katika mazoezi kwa sababu mchezo huo hautakuwa mwepesi kutokana na wapinzani wao kuzoea mazingira.

Kocha huyo alisema licha ya ushindi mnono wa mabao 4-0 walioupata katika mechi ya kwanza, hafurahishi na namba ambapo wachezaji wake wanavyopoteza nafasi za kufunga zinazotengenezwa.

Alisema ushindi walioupata katika mchezo wa kwanza sio kigezo cha wao kushinda mchezo wa kesho, wanatakiwa kupambana zaidi na kuongeza umakini ili kutumia vyema nafasi watakazozipata.

"Sio kwa sababu tulishinda katika mchezo wa kwanza, huu wa marudiano utakuwa mwepesi, tunatakiwa kuongeza umakini ikiwamo kuwajenga kisaikolojia wachezaji na kuamini utakuwa ni mchezo mgumu kuzidi ule wa awali," Nabi alisema.

Aliongeza wachezaji wanatakiwa kuingia uwanjani kwa makini kuhakikisha wanapata ushindi katika mchezo huu ambao ni muhimu ili waweze kufikia malengo yao.

# Simba yafunguka kazi imeanza

### ●●● Mgunda, wachezaji waahidi kuendelea kupambana kwa sababu Ligi Kuu...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Prisons katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya juzi, Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, amesema ameanza rasmi mbio za kuwania ubingwa wa ligi hiyo ya juu nchini.

**Mgunda aliliambia gazeti hili ushindi huo ni mwanzo wa mambo mazuri mbalimbali yanayotarajiwa kuonekana ndani ya kikosi chake ambacho kinajiandaa kuwakaribisha Nyasa Big Bullets katika mechi ya kimataifa ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa kesho kutwa.**

Hata hivyo kocha huyo alisema mechi hiyo dhidi ya Prisons ilikuwa ngumu kama walivyotarajia, lakini anashukuru wachezaji wake walipambana hadi dakika ya mwisho na hatimaye kuondoka na pointi tatu muhimu.

"Waliipigania nembo ya klabu na mashabiki. Tumshukuru Mungu mechi hii ngumu imeisha salama, ila niseme tu hakuna ligi nyepesi, hii ni ligi na watu washindani, mmeona Prisons walikuwa washindani wa kweli kweli, tunashukuru tumeshinda, tumepata alama tatu. Ugumu wake ulikuwa kwa sababu Prisons wana historia ya kuifunga Simba au kupata matokeo mazuri wakiwa hapa, kwa hiyo utaona timu imekuja kiushindani zaidi na wameshindana, niwapongeze wachezaji kwa hilo," alisema Mgunda.

Aliongeza kuhusu mabadiliko aliyofanya kwa kumtoa, Henock Inonga na kumwingiza, Joash Onyango alisema hayakuwa na kiufundi bali ya lazima kutokana na Inonga kupata matatizo ya misuli.

"Watu wengi hawaelewi, na mashabiki wanataka kuona kile wanachokiona, lakini Inonga tayari alikuwa ameshaumia, hivyo kuendelea kumchezesha ilikuwa ni kumuumiza na kumkosa katika mechi nyingine ngumu na muhimu huko mbele," Mgunda alisema.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema ushindi walioupata juzi umewapa furaha mashabiki wote wa klabu hiyo kwa sababu Prisons kama ilivyo kawaida yao wakicheza na Simba walionekana kuwa bora na kuonyesha ushindani wa kweli.

"Ni furaha kubwa kwa Wanasimba wote, ni pointi tatu tulizokuwa tunazihitaji, hii tafsiri halisi ya Ligi Kuu. Prisons walikuwa bora kwa tafsiri halisi ya ushindani, mambo yalikuwa magumu, imetulazimu kusubiri dakika nyingi, lakini hali ya upambanaji ya wachezaji wetu licha ya ugumu, lakini kupata ushindi Sokoine si jambo dogo, msimu uliopita tulifungwa. Ni ushindi ambao umetuweka vizuri kisaikolojia kuelekea mechi dhidi ya Nyasa Big Bullets," alisema meneja huyo.

Naye Onyango ambaye alicheza mechi ya kwanza msimu huu akiingia kipindi cha pili alikiri aliomba kuondoka katika klabu ya Simba kutokana kutokuwa katika mipango ya aliyekuwa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Zoran Maki, ambaye aliachana na timu hiyo hivi karibuni.

"Ni kweli niliomba kuondoka, sababu kocha mgeni aliyekuja nadhani sikuwa kwenye mipango yake, lakini sasa yamekwisha, leo (juzi), nimecheza, tuko na kocha mzuri (Mgunda), kwa hiyo tu inabidi wachezaji tumpe ushirikiano ili twende mbali," alisema Mkenya huyo.

Kocha Msaidizi wa Prisons, Shaaban Mtupa, mbali na kuwapongeza vijana wake kwa kufuata maelekezo hadi pale waliporuhusu bao dakika za lala salama alisema haikuwa bahati yao.

"Hatukuwa makini kwenye faulo iliyopigwa tukafungwa, lakini niseme tu mechi ilikuwa ngumu, kila timu ilicheza vizuri niwapongeze vijana wangu, pia Simba kwa kupata matokeo mazuri," Mtupa alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >